

—
SURA YA 345
—

SHERIA YA MIKATABA

[SHERIA KUU]

MPANGILIO WA VIFUNGU

Kifungu *Jina*

SEHEMU YA I
MASHARTI YA MWANZO

1. Jina fupi.
2. Tafsiri.

SEHEMU YA II
MAWASILIANO, KUKUBALIWA NA KUKATALIWA KWA PENDEKEZO

3. Mawasiliano, kukubaliwa na kufutwa kwa pendekezo.
4. Mawasiliano yanapokamilika.
5. Kufutwa kwa pendekezo na kukubaliwa kwake.
6. Kufutwa kunavyofanyika.
7. Kukubali lazima kuwe kwa uhakika.
8. Kukubali kwa kutimiza masharti, au kupokea malipo.
9. Ahadi ya wazi au ya kimazingira.

SEHEMU YA III
MIKATABA INAYOBATILIKA NA MAKUBALIANO BATILI

10. Makubaliano gani ni mikataba.
11. Watu wenye uwezo wa kufanya mikataba.
12. Akili timamu kwenye mikataba ni nini.
13. Tafsiri ya “Ridhaa”
14. Tafsiri ya “Ridhaa huru”.
15. Tafsiri ya “Shurutisho”
16. Tafsiri ya “Nguvu za uchocho”.
17. Tafsiri ya “Udanganyifu”.
18. Tafsiri ya “Kuwakilisha visivyo”.
19. Matokeo ya mikataba iliyosababishwa na shurutisho, udanganyifu, kuwakilisha visivyo au matumizi ya nguvu za uchocho.
20. Mkataba batili ikiwa wahusika wote wamekosea mambo muhimu.
21. Matokeo ya kukosea kisheria
22. Makosa yanayofanana.
23. Malipo ya vitu ambavyo ni halali na ambavyo siyo halali.
24. Makubaliano ni batili kama malipo na vitu siyo halali kw sehemu

25. Makubaliano bila malipo ni batili, isipokuwa tu kama yameandikwa na kusajiliwa; au ni ahadi ya kufidia kitu kilichofanywa; au ni ahadi ya kulipa deni lililozuiwa na ukomo wa kisheria.
26. Makubaliano ya kuzuia ndoa ni batili.
27. Makubaliano ya kuzuia biashara ni batili.
28. Makubaliano ya kuzuia mwenendo wa mahakama ni batili.
29. Makubaliano kuwa batili kwa kutokuwa wazi.
30. Makubaliano kwa njia ya kuwekewa dau ni batili.

**SEHEMU YA IV
MIKATABA ISIYO NA UHAKIKA**

31. Tafsiri ya “Mikataba isiyo na uhakika”.
32. Utekelezaji wa mikataba isiyo na uhakika tukio linapotokea.
33. Utekelezaji wa mikataba inayowezekana tukio liisipotokea.
34. Pale ambapo mkataba usio na uhakika unachukuliwa kushindikana, iwapo ni kitendo alichopanga mtu kukifanya baadae.
35. Mkataba usio na uhakika.
36. Mkataba usio wa uhakika kwa kitu kisichowezekana ni batili.

**SEHEMU YA V
UTEKELEZAJI WA MIKATABA**

Mikataba ambayo lazima itekelezwe

37. Wajibu wa wahusika katika mikataba.
38. Matokeo ya kukataa kupokea pendekezo la kutekelezwa.
39. Matokeo ya muhusika kukataa kutekeleza ahadi yote.
40. Watu ambao ahadi zinaweza kutekelezwa.
41. Matokeo ya kukubali utekelezwaji na mtu wa tatu.

Madhara na Haki za pamoja

42. Kuhamisha madeni ya pamoja.
43. Majukumu na madeni kwa watoa ahadi wa pamoja.
44. Matokeo ya kumwachilia mmoja kati ya watoa ahadi.
45. Kuhamisha kwa haki za pamoja.

Muda na Mahali pa Utekelezaji

46. Muda wa kutekeleza ahadi ikiwa hakuna maombi yaliyotolewa na muda haujapangwa.
47. Muda na mahali pa kutekeleza ahadi ikiwa muda umepangwa na hakuna maombi kufanywa.
48. Maombi ya kutekeleza ahadi kwa baadhi ya siku yawe na muda na mahali muafaka

49. Mahali pa kutekelezea ahadi ikiwa maombi hayajatolewa na hakuna makubaliano ya mahali pa utekelezaji.
50. Utekelezaji kwa namna au muda uliokubaliwa au kuwekwa na mtoa ahadi.

Utekelezaji wa ahadi za pamoja.

51. Mtoa ahadi halazimishwi kutekeleza isipokuwa tu kama mtoa ahadi mwenza yuko tayari na ana nia ya kutekeleza.
52. Amri ya kutekeleza ahadi za pamoja.
53. Madeni ha mhusika anayezuia tukio ambalo lingewezesha mkataba kutekelezeka.
54. Matokeo ya kushindwa kutekeleza ahadi ambayo ilitakiwa itekelezwe kwanza katika ahadi za pamoja.
55. Matokeo ya kushindwa kutekeleza kwa wakati uliowekwa katika mkataba.
56. Makubaliano ya kufanya kitendo kisichowezekana, chenye ugumu au kisicho halali na fidia husika.
57. Ahadi za pamoja za kufanya vitu halali, na pia vitu vingine visivyo halali.
58. Ahadi mbadala, sehemu mojawapo kuwa si halali.

Kujitengea Malipo

59. Maombi ya malipo ikiwa deni linalotakiwa kulipwa limeonyeshwa.
60. Maombi ya malipo ikiwa deni linalotakiwa kulipwa halijaonyeshwa.
61. Maombi ya malipo ikiwa hakuna mhusika aliyejitengea malipo.

Mikataba Ambayo Haitakiwi Kutekelezwa

62. Matokeo ya kuhuishwa, kabilishwa na kubadilishwa kwa mkataba.
63. Mpokea ahadi anaweza kuacha ama kutekeleza ahadi.
64. Matokeo ya kubatilisha mkataba unaoweza kubatilika.
65. Wajibu wa mtu aliyenufaika kwa mkataba batili au mkataba unaoweza kubatilika.
66. Jinsi ya kutoa taarifa juu ya kufuta ubatilishaji wa mkataba unaoweza kuwa batili.
67. Matokeo ya uzembe wa mtoa ahadi.

SEHEMU YA VI
MAHUSIANO FULANIYANAYOFANANA NA YALE YALIYOTOKANA NA
MKATABA

68. Madai muhimu ya huduma aliyopewa mtu asiyestahili kuingia mkataba au kwa ajili yake mwenyewe.
69. Marejesho ya pesa kwa aliyelipa ikiwa ni malipo yenye manufaa kwake.
70. Wajibu wa mtu aliyefurahia manufaa ya vitendoambavyo si vya bure.
71. Majukumu ya aliyefichua mali.

72. Deni la mtu ambaye pesa au mzigo vimelipwa kwake kwa makosa au kwa lazima.

SEHEMU YA VII
MATOKEO YA KUVUNJA MKATABA

73. Fidia kwa hasara au uharibifu uliosababishwa na kuvunjika kwa mkataba.
74. Fidia kwa kuvunjika kwa mkataba pale ambapo adhabu inajulikana.
75. Mhusika anayebatilisha kihalali mkataba anastahili fidia.

SEHEMU YA VIII
FIDIA BIMA NA DHAMANA

76. Tafsiri ya "Mkataba wa Fidia Bima".
77. Haki za mwenye fidia bima akishitakiwa n.k.
78. Tafsiri ya "Mkataba wa udhamani", "mdhamini" "mdaiwa mkuu" na "mkopeshaji".
79. Malipo ya udhamini.
80. Deni la mdhamini.
81. Tafsiri ya "Dhamana endelevu".
82. Kufutwa kwa dhamana endelevu.
83. Kufutwa kwa dhamana endelevu kutokana na kifo cha mdhamini.
84. Deni la watu wawili, wenye deni la msingi, halitavurugwa na mipango yao kwamba mmoja atakuwa mdhamini dhidi ya mwingine.
85. Kuachiwa kwa mdhamini kutokana na kubadilika kwa masharti ya mkataba.
86. Kuachiwa kwa mdhamini kutokana na kuachiwa kwa mdaiwa mkuu.
87. Kuachiwa kwa mdhamini wakati mkopeshaji atakapojipa muda, na kuamua kuto kumshitaki mdaiwa mkuu.
88. Mdhamini haachiwi kama makubaliano yamefanywa na mtu mwingine na kumpa muda mdaiwa mkuu.
89. Msamaha wa mkopeshaji kufungua mashitaka hakumuachi huru mdhamini.
90. Kuachiwa kwa mdhamini mwenza hokusababishi wengine kuachiwa.
91. Kuachiwa kwa mdhamini kunakosababishwa na mmkopeshaji kunapelekea mdhamini kupata nafuu.
92. Haki za mdhamini kuhusu malipo au kutekelezwa kwa mkataba.
93. Haki ya mdhamini kuwanufaisha wadhamini wa mkopeshaji.
94. Udhamini unaopatikana kwa uwakilishi wa uongo si halali.
95. Udhamini anaopatikana kwa mbinu si halali.
96. Udhamani katika mkataba ambao mkopeshaji hawezi kufanya chochote hadi wadhamini wenza wajiunge.
97. Ahadi ya kumaanisha kumfidia mdhamini.
98. Wadhamini wenza kupaswa kulipa sawa.
99. Madeni ya wadhamini wenza kufungwa kwa kiasi tofauti.

SEHEMU YA IX
DHAMANA

100. Tafsiri ya "Dhamana", "mdhamini" na "mdhaminiwa".
101. Jinsi ambavyo mdhaminiwa anapelekewa bidhaa.
102. Wajibu wa mdhamini kutoa dosari katika bidhaa zilizodhaminiwa.
103. Uangalifu anaopaswa kuwa nao mdhaminiwa.
104. Wakati ambapo mdhaminiwa hawajibiki n.k. kwa kitu kilichodhaminiwa –rehani.
105. Kusitishwa kwa dhamana kutokana na kitendo cha mdhaminiwa kilicho kinyume na masharti.
106. Wajibu wa mdhaminiwa aliyeruhusu matumizi ya bidhaa zilizowekwadhamana.
107. Matokeo ya mchanganyiko, kwa ridhaa ya mdhamini jyy ya bidhaa zake na za mdhaminiwa.
108. Matokeo ya mchanganyo, bila ya ridhaa ya mdhamini ikiwa bidhaa zinaweza kuchanganuliwa.
109. Matokeo ya mchanganyiko, bila ya ridhaa ya mdhamini ikiwa bidhaa haziwezi kuchanganuliwa.
110. Malipo ya gharama za lazima afanyayo mdhamini.
111. Kurudishwa kwa bidhss zilizoainishwa bila malipo.
112. Kurudishwa kwa bidhaa zilizowekewa dhamana muda wake unapokwisha au madhumuni yake kutimia.
113. Wajibu wa mdhaminiwa ikiwa bidhaa hazijarudishwa.
114. Kukatishwa kwa dhamana isiyo na malipo kwa kifo.
115. Mdhaminiwa anastahili ongezeko au faida kutokana na mali iliyowekwa dhamana.
116. Wajibu wa mdhamini kwa mdhaminiwa.
117. Dhamana ya wadhamini wenza.
118. Mdhaminiwa hawajibiki kwa mdhamini hewa
119. Haki ya mtu wa tatu anayedai bidhaa zilizowekwa dhamana.
120. Haki ya aliyefichua bidhaa.
121. Wakati ambapo aliyefichua bidhaa inayouzika anapoweza kuiuza.
122. Wakati ambapo deni la mshika bidhaa za rehani litakapolipwa.
123. Wakati mtumishi wa benki anaposhikilia bidhaa kama rehani

Ahadi za Dhamana

124. Tafsiri ya "ahadi", "mtoa rehani", and "muweka rehani".
125. Haki ya kushikilia bidhaa ya muweka rehani.
126. Muweka rehani kutoshikilia kwa ajili ya deni au ahadi zaidi ya zile zilizowekewa ahadi.

Dhana ya Maombi ya Nyongeza

- 127. Haki ya mtoa rehani ikiwa kuna gharama za nyongeza.
- 128. Haki ya muweka rehani ikiwa atakosea.
- 129. Haki ya kudai ya muweka rehani aliyekosea.
- 130. Ahadi ya wakala wa biashara na mwenye mali katika mkataba batili.
- 131. Ahadi ikiwa muweka rehani ana faida ndogo.

Mashauri ya Mdhamini au Mdhaminiwa dhidi ya waovu

- 132. Shauri la mdhamini au mdhaminiwa dhidi ya waovu.
- 133. Mgawanyo wa nafuu au fidia iliyopatikana katika mashauri hayo.

SEHEMU YA X
UWAKALA

Uteuzi na Mamlaka ya mawakala

- 134. Tafsiri ya "Wakala" na "mhusika mkuu"
- 135. Nani anaweza kuajiri wakala.
- 136. Nani anaweza kuwa wakala.
- 137. Malipo siyo muhimu.
- 138. Mamlaka ya wakala yaweza kuwa ya kutajwa wazi wazi au ya kumaanisha.
- 139. Tafsiri ya mamlaka ya kutajwa waziwazi au ya kumaanisha.
- 140. Ukubwa wa mamlaka ya wakala.
- 141. Mamlaka ya wakala wakati wa dharura.

Msaidizi wa wakala

- 142. Wakati ambapo wakala hawezi kukasimu.
- 143. Tafsiri ya "Msaidizi wa wakala".
- 144. Uwakilishi wa mhusika mkuu na msaidizi wa wakala aliyeteuliwa.
- 145. Jukumu la wakala kwa msaidizi wake ambaye hakuteuliwa na mamlaka.
- 146. Uhusiano kati ya mhusika mkuu na mtu aliyeteuliwa kuwakilisha shughuli za wakala.
- 147. Wajibu wa wakala kumtaja aliyeteuliwa.

Uthibitisho

- 148. Haki ya mtu ambaye amefanyiwa kitendo bila ya ridhaa yake na matokeo ya uthibitisho.
- 149. Uthibitisho unaweza kuwa wa wazi au wa kimazingira
- 150. Ujuzi unaohitajiwa kwa uthibitisho.
- 151. Matokeo ya uthibitisho wa matendo yasiyoruhusiwa yakiwa ni sehemu ya mkataba.
- 152. Uthibitisho wa matendo yasiyoruhusiwa hauwezi kumdhuru mtu wa tatu.

Kufutwa kwa Uwakala

153. Kusitishwa kwa uwakala.
154. Kusitishwa kwa uwakala, ikiwa wakala ana maslahi katika suala husika.
155. Wakati ambao mhusika mkuu anaweza kufuta mamlaka ya wakala.
156. Ufutaji ikiwa mamlaka yametokelezwa nusu.
157. Fidia kwa ufutaji uliofanywa na mhusika mkuu au kujitoa kwa wakala.
158. Taarifa ya ufutaji au rudisho.
159. Ufutaji na rudisho vyaweza kuwa vya kutajwa wazi au kwa kumaanisha.
160. Wakati ambapo kusitishwa kwa mamlaka ya wakala kutaleta matokeo kwa wakala, na kwa mtu wa tatu.
161. Jukumu la wakala wakati wa kusitisha uwakala kutokana na kifo au ulemavu wa akili wa mhusika mkuu .
162. Kusitishwa kwa mamlaka ya wakala msaidizi.

Wajibu wa Wakala kwa Mhusika Mkuu

163. Wajibu wa wakala katika kutekeleza shughuli za mhusika mkuu.
164. Ujuzi na uadilifu unaotakiwa kwa wakala.
165. Akaunti ya wakala.
166. Jukumu la wakala la kuwasiliana na mhusika mkuu.
167. Haki ya mhusika mkuu wakati wakala akifanya kazi, bila ridhaa ya mhusika mkuu.
168. Haki ya mhusikakatika manufaa aliyoyapata wakala katika shughuli zake za uwakala.
169. Haki ya wakala ya kubakiza pesa kwenye akaunti ya mhusika mkuu.
170. Wajibu wa wakala kulipa pesa iliyopatikana kwa mhusika mkuu.
171. Wakati malipo ya wakala yanapokuwa tayari.
172. Wakala hastahili malipo kwa shughuli aliyoharibu.
173. Rehani ya wakala kwa mali ya mhusika mkuu.

Wajibu wa Mhusika Mkuu kwa Wakala

174. Wakala anatakiwa afidiwe kwa shughuli halali anazozifanya kwa nia njema.
175. Wakala anatakiwa afidiwe dhidi ya matendo yaliyofanywa kwa nia njema.
176. kutowajibika kwa mwajiri wa wakala kufanya jinai.
177. Fidia kwa madhali aliyoyapata wakala kutokana na uzembe wa mhusika

Matokeo ya Uwakala kwenye Mikataba na mtu wa Tatu.

178. Utekelezaji na matokeo ya mikataba ya uwakala.
179. Nafasi ya mhusika mkuu wakala anapovuka mipaka ya mamlaka.
180. Mhusika mkuu, halazimiki ikiwa uvukaji mipaka wa wakala ulikuwa hautengeki.

181. Matokeo ya taarifa apewayo wakala.
182. Wakala kwa nafasi yake hawezi kulazimishwa wala kubanwa na mikataba kwa niaba ya mhusika mkuu.
183. Haki ya wahusika katika mkataba uliofanywa na wakala hazitakiwi kuwekwa bayana.
184. Haki ya mtu anayefanya kazi na wakala ni wake binafsi.
185. Matokeo ya kumtumia wakala au mhusika mkuu.
186. Uwajibikaji wa wakala anayeigiza.
187. Mtu mwenye mkataba wa uongo wa uwakala hastahili kuhusishwa na utekelezaji.
188. Uwajibikaji wa mhusika mkuu kwa kulazimisha imani kwamba wakala aliruhusiwa kufanya vitendo alivyovifanya bila ruhusa.
189. Matokeo katika makubaliano ya uwakilishaji wa uongo au udanganyifu au yafanywayo na wakala.

SEHEMU YA XI UBIA

Aina za Ubia

190. Tafsiri ya "Ubia" na "ushirika".
191. Kanuni za kujulisha kuwepo kwa ubia.

Mahusiano baina ya Wabia

192. Majukumu ya jumla ya wabia.
193. Ridhio la kutofautiana katika masharti ya ubia.
194. Ufanyaji wa shughuli na haki za msingi na majukumu.
195. Mali za ubia.
196. Jukumu la wabia katika faida binafsi na ushindani wa biashara.
197. Neno ubia linapokosa nguvu.
198. Utambulisho wa wabia wapya.
199. Kukataliwa
200. Kustaafu.

Mahusiano ya Wabia kwa wanaofanya nao kazi

201. Nguvu ya wabia kufunga shirika.
202. Wabia kufungwa na vitendo vyao kwa niaba ya shirika.
203. Jukumu la wabia kuhusiana na madeni.
204. Deni kwa makosa na matumizi yasiyo halali
205. Matumizi mabaya ya mali ya amana kwa manufaa ya ubia.
206. Kosa la kujifanya mtu wa madaraka.
207. Taarifa kwa wabia kuwa taarifa kwa shirika.
208. Madeni kwa wabia wanaoondoka na wanaojiunga.

- 209. Ufutaji wa wadhamini endelevu kwa kubadili jina la shirika.
- 210. Haki ya waliogawa sehemu katika ubia.
- 211. Watoto hawaruhusiwi kuwa wabia.

Kuvunjika kwa Ubia na Matokeo yake

- 212. Kuvunjika kutokana na kwisha kwa muda au kwa kutoa taarifa.
- 213. Kuvunjika kutokana na kifo au kufilisika.
- 214. Kuvunjika kwa ubia kinyume na sheria.
- 215. Ukomokwa amri ya mahakama.
- 216. Haki ya watu dhidi ya wajumbe dhahiri wa shirika .
- 217. Haki ya wabia ya kupata taarifa ya kuvunjika ubia.
- 218. Muendelezo wa haki na madeni kwa wabia baada ya kuvunjika kwa ubia..
- 219. Haki ya mbia katika maombi ya mali za wabia.
- 220. Uteuzi wa msimamizi ikiwa ubia umevunjika.
- 221. Haki ikiwa ubia umevunjika kwa udanganyifu au uwakilishi mbaya
- 222. Haki ya mbia anayeondoka katika mazingira fulani kuhusiana na faida iliyopatikana baada ya kuvunjika kwa ubia.
- 223. Sehemu ya mbia aliye staafu au kufariki itakuwa deni.
- 224. Kanuni kuhusiana na mgawanyo wa mali baada ya kufunga akaunti.
- 225. Ulipaji wa madeni ya shirika na madeni mengine.
- 226. Ubia wa pamoja na makampuni yaliyoungana.

SEHEMU YA XII
KUFUTWA KWA SHERIA NAVIFUNGU VYA MPITO

- 227. [Kutotumika kwa Sheria ya Mikataba ya India na marekebisha yake Sura ya 2.]
- 228. [Vifungu vya mpito.]

SURA YA 345

SHERIA YA MIKATABA

Sheria inayohusiana na mikataba.

[3 Machi, 1961]

Shr. Na. 1 ya 1961
[R.L. Sura. 433]
Sheria Na. 55 ya 1963

SEHEMU YA I
VIFUNGU VYA AWALI

Jina fupi

1.-(1) Sheria hii inaweza kuitwa Sheria ya Mikataba.

(2) Yaliyomo katika Sheria hii hayatadhuru vifungu vya sheria yoyote inayotumika Tanzania, na ambayo haijsemwa waziwazi kutotumika au kufutwa na pia utumiaji wowote au desturi ya biashara, wala tukio lolote la mkataba wowote ambao uko kinyume na masharti ya Sheria hii.

Tafsiri
Sheria Na. 55 ya
1963 Jdw

2.-(1) Katika Sheria hii, isipokuwa kama maudhui yatahitaji vinginevyo–

- (a) mtu anapoonyesha kwa mtu mwingine uhiyari wa kufanya kitu au kutofanya, kwa lengo la kuungwa mkono na mtu huyo kwa, kitendo au kutotenda,atachukuliwa kutoa pendekezo.
- (b) mtu ambaye anapendekezewa, akaonyesha kuunga mkono, inasemekana pendekezo limekubalika, na pendekezo linapokubalika, inakuwa ni ahadi;
- (c) mtu anayetoa pendekezo anaitwa "mtoaji", na anayekubali pendekezo anaitwa "mpokeaji";
- (d) ikiwa, kwa hiyari ya mtoaji, mpokeaji au mtu mwingine yeyote ametenda au hakufanya, au ameahidi kufanya au kutofanya, au amefanya au hajafanya, kitu fulani, kitendo au ahadi hiyo inaitwa malipo ya ahadi;
- (e) kila ahadi na kila fungu la ahadi inayo tolewa, inayounda malipo baina yao ni makubaliano;
- (f) ahadi zinazosababisha malipo ya ahadi baina ya pande mbili zinaitwa ahadi pacha;
- (g) makubaliano ambayo hayana nguvu kisheria yanatambulika kuwa ni batili;
- (h) makubaliano ambayo yana nguvu kisheria ni mkataba;
- (i) makubaliano ambayo yana nguvu kisheria, kwa ridhaa ya upande mmoja au zaidi bila ya kuhusisha mwingine ni batili;
- (j) mkataba ambao unashindikana kutekelezwa kisheria unakuwa batili.

(2) Bila kujali aya ya (g) au (j) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, wakati sheria hii inaanza kutumika Tanzania, kuna sheria nyingine yoyote inasema makubaliano yoyote hayatakuwa na nguvu mpaka masharti fulani yatimizwe, au ridhaa ipatikane, makubaliano hayo hayatakuwa batili kwa sababu ya kuto kutekelezwa kwake katika sheria hiyo,kwa kutaka kutimizwa kwa hitaji hilo au kupatikana kwa ridhaa hiyo.

(3) Hakuna kitu chochote katika sheria hii, mbali na kifungu cha 23, kitadhuru sheria ya mila; na katika hali yoyote ikiwa sheria inayotumika ni sheria ya mila, kifungu cha 23 kinakuwa ni nyongeza katika kanuni za mila na rejeo katika kifungu cha 23 itachukuliwa ni rejeo katika sheria za Tanzania.

SEHEMU YA II

MAWASILIANO, KUKUBALIWA NA KUFUTWA KWA PENDEKEZO

Mawasiliano,
kukubaliwa na
kufutwa kwa
pendekezo

3. Mawasiliano, kukubaliwa na kufutwa kwa pendekezo, vinasemekana kufanyika kwa kitendo chochote, kinachofanywa na mhusika unaotoa, anayekubali au kufuta toleo, akiwa anakusudia kutoa taarifa ya mawasiliano ya pendekezo kukubalika au kufutwa na ambalo litakuwa na matokeo ya kuliwasilishwa..

Mawasiliano
yanapokamilika

4.-(1) Mawasiliano ya toleo yanakamilika pale ambapo yanamfikia aliyekusudiwa.

(2) Mawasiliano ya kukubali yanakamilika-

- (a) kwa upande wa mtoa pendekezo, pale majibu yanapokuwa njiani kumfikia kutoka kwa mpokeaji;
- (b) kwa upande wa mpokeaji, pale majibu yanapomfikia mtoa pendekezo.

(3) Mawasiliano ya kukataa yanakamilika-

- (a) kwa mhusika wa aliyekataa, pale ambapo taarifa inakuwa njiani kuelekea kwa mlengwa, nakuwa nje ya uwezo wa aliyekataa;
- (b) kwa mhusika wa anayesubiri majibu, pale ambapo taarifa inamfikia.

Kufutwa kwa
pendekezo na
kukubaliwa kwake

5.-(1) pendekezo linaweza kufutwa wakati wowote kabla mawasiliano ya kukubali hayajakamilika kwa mhusika wa aliyetoapendekazo, na sio baada ya hapo.

(2) Kukubali pendekazo kunaweza kukataliwa wakati wowote kabla mawasiliano ya kukubali hayajakamilika kwa mhusika aliyekubali, na sio baada ya hapo.

Kufutwa
kunavyofanyika

6. Pendekazo linafutwa-

- (a) kwa mawasiliano ya taarifa ya kufutwa kutoka kwa mtoaji wa pendekazo kwenda kwa mpokeaji;
- (b) kuisha kwa muda wa kukubaliwa kulikokusudiwa kwenye toleo husika, au, kama hakuna muda uliopangwa basi muda mrefu ukipita bila ya kukubaliwa;
- (c) kwa mpokeaji kushindwa kutimiza masharti yaliyoongozana na pendekazo; au
- (d) kwa kifo au kupata wazimu kwa mtowa pendekazo, kama taarifa ya kifo au wazimu itamfikia anayekubali kabla hajakubali.

Kukubali lazima
kuwe kwa uhakika

7. Ili kubadilisha pendekazo kuwa ahadi, ukubali unatakiwa-

- (a) uwe sahihi, kamili na wa uhakika;
- (b) uwe umeelezewa katika hali ya kawaida na inayoeleweka,

labda tu kama toleo limeelekeza ni kwa jinsi gani litakubalika; na kama pendekezo limeelekeza jinsi ya kukubali na ukubali haukufuta maelekezo hayo, muda mfupi baada ya ukubali kumfikia mtoa pendekezo, anaweza kuisitiza kuwa ukubali lazima ufanyike kuligana na maelekezo na siyo vinginevyo, ikishindikana mtoa pendekezo atakubali.

Kukubali kwa kutimiza masharti au kupokea malipo

8. Kutimiza masharti ya pendekezo, au kukubali malipo yoyote baina ya watoaji ambayo yanaweza kutolewa na pendekezo, ni kukubali pendekezo.

Ahadi ya waziwazi au ya kimazingira

9. Ikiwa pendekezo au ukubali wa ahadi umefanyika kwa maneno, ahadi inasemekana ni ya wazi wazi; na ikiwa pendekezo au ukubali umefanyika kwa njia nyingine mbali na maneno, ahadi inasemekana ni ya kimazingira.

SEHEMU YA III MIKATABA INAYOBATILIKA NA MAKUBALIANO BATILI

Makubaliano gani ni mikataba.

10. Makubaliano yote ni mikataba kama yatakuwa yamefanywa kwa hiari na watu wanaostahili kufanya makubaliano, kwa malipo ya kitu halali na ambayo hayajatajwa waziwazi hapa kuwa ni batili:

Isipokuwa kwamba maelezo yoyote yaliyomo hayatadhuru sheria yoyote inayotumika, na ambayo imefutwa ama kuacha kutumika, inayoelekeza mikataba yote inatakiwa iwe kwenye maandishi au ifanywe mbele ya mashahidi, au sheria yoyote ihusuyo usajili wa nyaraka.

Watu wenye uwezo wa kufanya mikataba.

11.-(1) Kila mtu mwenye umri wa mtu mzima na mwenye akili timamu, ambaye hajazuiwa na sheria yoyote, anau wezo wa kuingia mkataba.

(2) Makubaliano yanayofanywa na mtu ambaye hajatangazwa hapa kuwa na uwezo wa kufanya mkataba, hayo kisheria ni batili.

Akili timamu kwenye mikataba ni nini.

12.-(1) Katika kufanya mkataba, mtu anasemekana kuwa na akili timamu wakati wa kufanya mkataba ikiwa ana uwezo wa kuelewa na kutafakari maslahi yake katika mkataba husika.

(2) Mtu ambaye mara nyingi anakua na matatizo ya akili, lakini muda mfupi anakuwa timamu, anaweza kufanya mkataba wakati anapokuwa na akili timamu.

(3) Mtu ambaye mara nyingi anakuwa na akili timamu, lakini muda mfupi anakuwa na matatizo ya akili, hawezi kufanya mkataba muda anaokuwa na matatizo ya akili.

Tafsiri ya "Ridhaa" **13.** Watu wawili au zaidi wanasemekana wameridhia pale wanapokubaliana kitu kimoja kwa maana sawa.

Tafsiri ya "Ridhaa huru" **14.**-(1) Kuridhia kunasemekana ni huru ikiwa hakujasababishwa na-
(a) shurutisho, kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 15;
(b) nguvu za uchocheo kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 16;
(c) udanganyifu, kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 17;
(d) kuwakilisha visivyo, kama ilivyotafsiriwa katika kifungu cha 18; au
(e) makosa kulingana na vifungu vya 20, 21 na 22.

(2) Ridhaa inasemekana kuwa siyo huru kama itakuwa imetolewa chini ya shurutisho, uchochezi, udanganyifu, uwakilishi wa uongo au kwa makosa/kukosea.

Tafsiri ya "Shurutisho" Sura ya .16 **15.**-(1) "shurutisho" ni kutenda au kutishia kutenda kosa ambalo limekatanzwa chini ya sheria ya Kanuni ya Adhabu, au kuzuia au kutishia kuzuia kitu ili kumrubuni mtu aingie kwenye mkataba.

Sura ya 16 (2) Kwa madhumuni ya Sheria hii, haijalishi kama sheria ya Kanuni ya Adhabu inatumika au la katika eneo ambalo shurutisho limefanyika.

Tafsiri ya "Nguvu za uchocheo" **16.**-(1) Mkataba unasemekana kuwa umechochewa pale ambapo mahusiano baina ya wahusika ni kwamba mmoja ana nafasi ya kutawala hiari ya mwingine na kutumia nafasi hiyo vibaya kwa faida yake.

(2) Kwa namna ya pekee na bila kuathiri kanuni hiyo iliyotangulia mtu anasemekana kutawala hiari ya mwingine-

- (a) pale anapokuwa na madaraka ya wazi juu ya mwingine, au pale ambapo kunauhusiano wa kuaminiana; au
- (b) pale ambapo anafanya mkataba na mtu ambaye ana matatizo ya akili ya kudumu au ya muda yaliyosababishwa na umri mkubwa, maradhi au uchovu wa akili au mwili.

(3) Pale ambapo mtu ana nafasi ya kutawala hiari ya mwingine, anaingia nae mkataba, na tukio hilo linaonekana machoni pa watu au ushahidi uliotolewa kuwa kitendo hicho hakipingiki, mwenye jukumu la kuthibitisha kuwa mkataba huo haukutokana na uchochezi ni la yule mtu mwenye nafasi ya kutawala hiari ya mwingine:

Sura ya.6 Isipokuwa kwamba hakuna kitu chochote katika kifungu kidogo kitaingilia kifungu cha 120 cha Sheria ya Ushahidi .

Tafsiri ya "Udanganyifu" **17.**-(1) "Udanganyifu" maana yake ni moja kati ya vitendo vifuatavyo vinavyotendwa na mhusika katika mkataba kwa usiri au kupitia wakala wake, kwa nia ya kumlaghai mhusika mwingine au wakala

wa upande ule au kumshawishi aingie katika mkataba-

- (a) mapendekezo kwa jambo la hakika kwa mambo ambayo si ya kweli na yule asiyeamini kuwa ni ya kweli;
- (b) kuficha ukweli na yuule mwenye kujua au kuamini kuhusu jambo analolijua;
- (c) kutoa ahadi ambayo haina nia ya kutekelezwa;
- (d) kitendo chochote kinachofaa kudanganya; au
- (e) kufanya chochote au kutofanya kitu ambacho sheria inaelekeza ni udanganyifu.

(2) Kwa madhumuni ya Sheria hii, kukaa kimya kuhusu jambo fulani linaloweza kudhuru hiari ya mtu kuingia katika mkataba sio udanganyifu, labda kama mazingira ya kesi ni ya kuhitaji mtu aliye kimya azungumze au ukimya wake ni sawa na kuzungumza.

Tafsiri ya
"Kuwakilisha
visivyo"

18."Kuwakilisha visivyo" maana yake ni-

- (a) utetezi wa nyongeza wa kitu tofauti na inavyofanywa na mtu, akijua ni kweli wakati sio kweli;
- (b) kuto tekeleza jukumu ambapo, bila ya kuwa na nia ya kudanganya, unapata faida kutokana na mtu kufanya hivyo au kitu kinachodaiwa kwake, kwa kumpotezea mtu mwingine uvumilivu;
- (c) kusababisha japo kwa nia njema, mtu kufanya makosa katika jambo muhimu katika makubaliano.

Matokeo ya
mikataba
iliyosababishwa na
shurutisho,
udanganyifu
kuwakilisha visivyo
au matumizi ya
nguvu za uchocheo.

19.-(1) Pale ambapo ridhaa katika mkataba inasababishwa na shurutisho, uchochezi, udanganyifu, au uwakilishi usio sahihi, makubaliano hayo ni mkataba batili kwa upande wa mtu ambaye ridhaa ilisababishwa na vichocheo hivyo:

Isipokuwa kwamba kama ridhaa hiyo ilisababishwa na uwakilishi usio halali au ukimya, au udanganyifu chini ya kifungu cha 17, mkataba hautakuwa mkataba unaobatilika kama mhusika katika mkataba aliyetoa ridhaa yake alikuwa na uwezo wa kugundua mbinu hizo.

(2) Udanganyifu au uwakilishi usivyo ambao haukusababisha ridhaa kwa mhusika aliyedanganywa au kwa mhusika ambaye uwakilishi usio halali ulifanywa, hausababishi mkataba kuwa mkataba unaobatilika

(3) Kama ataona inafaa, mhusika katika mkataba ambaye anaona ridhaa yake imesababishwa na udanganyifu au uwakilishi usivyo anaweza akiona inafaa kuisisitiza mkataba utekelezwe naye awe na nafasi ile ambayo angekuwa nayo kama uwakilishi ule ungekuwa ni kweli.

(4) Mkataba ambao unabatilika kwa kigezo kwamba ridhaa ya mhusika ilipatikana kwa uchochezi, unaweza kutupiliwa mbali, au kama mhusika aliyestahili kuepuka amenufaika kwa masharti ya mahakama kama itakavyona kufaa.

Mkataba batili ikiwa wahusika wote wamekosea mambo muhimu.

20.-(1) Pale ambapo wahusika wote katika makubaliano wamekosea katika jambo la ukweli lililo muhimu katika makubaliano, makubaliano yanayokuwa ni batili.

(2) Maoni yaliyokosewa kuhusu thamani ya kitu muhimu katika makubaliano hayatahesabiwa kama ni makosa kwa jambo la **ukweli**.

Matokeo ya kukosea kisheria.

21. Mkataba si mkataba unaobatilika kwa sababu ya kosa la kisheria inayotumika Tanzania; lakini kosa la kisheria ambayo haitumiki Tanzania ina matokeo sawa na kukosewa kwa jambo la ukweli.

Makosa yanayofanana

22. Mkataba hauwi mkataba unaobatilika kwa sababu tu ulisababishwa na mhusika mmoja kukosea kwa jambo la ukweli

Malipo ya vitu halali na ambavyo siyo halali.

23.-(1) Malipo au kitu kilicho katika makubaliano ni halali, isipokuwa kama-

- (a) inakatazwa na sheria;
- (b) mkataba huo jinsi ulivyo, kama utaruhusiwa utaathiri vifungu vya sheria yoyote;
- (c) ni wa udanganyifu;
- (d) yanajumuisha au kuonekan kumuumiza mtu au kuharibu mali ya mwingine; au
- (e) mahakama inaona makubaliano hayo kuwa kinyume na maadili au sera ya umma.

(2) Katika kila suala lililotajwa katika kifungu kidogo cha (1), malipo au kitu cha makubaliano kinasemekana sio halali; na kila makubaliano ambayo kitu ama malipo si halali ni batili na hakuna shauri litakalofunguliwa kudai pesa yoyote au mali au fidia kwa kitu chochote kilichofanywa katika makubaliano hayo, isipokuwa-

- (a) mahakama inaridhika kwamba mlalamikaji hakuwa na ufahamu juu ya uharamu wa malipo au kitu cha makubaliano wakati akitoa pesa au kitu kilichotakiwa kutolewa au amefanya kitu ambacho fidia inatafutwa au amefanya vitu hivyo ikiwa ni sehemu ya kukubali, na malipo au kitu ambacho ni haramu hakijatekelezwa wakati mdai alipotambua uharamu na makubaliano;
- (b) mahakama inaridhika kwamba ridhaa ya mlalamikaji kwenye makubaliano husika ilisababishwa na udanganyifu, uwakilishi usivyo, nguvu au uchochezi; au
- (c) makubaliano yametangazwa na sheria yoyote kuwa si halala kwa lengo la kuwalinda watu wa daraja fulani la maisha ambalo mlalamikaji yumo.

Makubaliano ni batili kama malipoya awali na

24. Iwapo sehemu yoyote ya malipo kwa kitu kimoja au zaidi, au sehemu moja au sehemu yoyote ya malipo kwa kitu kimoja si halala, makubaliano yanakuwa batili.

vitu siyo halali kwa sehemu

Makubaliano bila ya malipo ni batili, isipokuwa tu kama yameandikwa na kusajiliwa; au ni ahadi ya kufidia kitu kilichofanywa; au ni ahadi ya kulipa deni lililozuiwa na sheria ya ukomo

25.-(1) Makubaliano yanayofanywa bila ya malipo ni batili isipokuwa-

(a) yamewekwa katika maandishi na kusajiliwa chini ya sheria inayotumika ya kusajili nyaraka kwa wakati huo, na yamefanyika kwa mapenzi ya kawaida baina ya watu wenye uhusiano wa karibu.

(b) ni ahadi ya kutoa fidia yote au sehemu kwa mtu ambaye tayari amekwishafanya kitu kwa mtoa ahadi, au kwa kitu ambacho mtoa ahadi alilazimika kisheria kukifanya; au

(c) ni ahadi, iliyowekwa kwa maandishi na kusainiwa na mhusika, au wakala wake, ahadi ya kulipa kitu chote au sehemu ya deni ambalo mdai angeweza kulazimisha malipo ila kushindwa kulingana na Sheria ya Ukomo wa Mashauri,

katika moja kati ya mambo yaliyotajwa chini ya aya ya (a), (b) na (c), makubaliano ya aina hiyo ni mikataba.

(2) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitakacho athiri uhalali wa zawadi iliyotolewa baina ya mtoaji na mpokeaji.

(3) Makubaliano ambayo ridhaa ya mtoa ahadi ilikuwa huru hayawezi kuwa batili kwa sababu tu malipo au makubaliano hayajitoshelezi; lakini kutojitosheleza kwa malipo kutatiliwa maanani na mahakama wakati ikiamua swali kama ridhaa ya mtoa ahadi ilikuwa huru.

Makubaliano ya kuzuia ndoa ni batili/

26. Makubaliano yote yanayolenga kuzuia ndoa ya mtu yeyote, ambaye siyo mtoto, ni batili.

Makubaliano ya kuzuia biashara ni batili

27.-(1) Makubaliano yote ambayo yanamzuia mtu yeyote kutekeleza ueledi wake kisheria au kufanya biashara kwa kiasi ni batili, isipokuwa tu kama zuiu lina manufaa kwa wahusika katika mkataba na ni kwa manufaa ya umma.

(2) Kwa namna ya pekee na bila ya kuathiria kanuni iliyotangulia, makubaliano ya kuzuia biashara hayatakuwa na manufaa kwa wahusika kwenye makubaliano, iwapo zuiu linazidi kile ambacho ni muhimu katika kulinda maslahi ya wapokeaji.

(3) Jukumu la kuthibitisha kwamba zuiu lolote kuhusiana na maslahi ya wahusika ni la mpokeaji, na jukumu la kuthibitisha kwamba zuiu lolote si la kawaida kuhusiana na kulinda maslahi ya jamii ni la mtoaji.

Makubaliano ya kuzuia mwenendo wa mahakama ni batili/

28. Makubaliano yote, ambayo mhusika yeyote anazuiwa kudai haki yake chini ya mkataba kwa utaratibu wa kawaida wa mahakama, au yanayopunguza muda wa mhusika kudai haki hiyo, ni batili kwa kiasi hicho:

Isipokuwa kwamba kifungu hiki -

- (a) hakitasababisha uharamu wa -
 - (i) mkataba ambao watu wawili au zaidi wamekubaliana kwamba mgogoro wowote utakaotokea baina yao utapelekwa kwenye usuluishi, na kwamba kiasi kile tu kitakachotolewa kwenye usuluhishi ndicho kitakacholipwa kuhusiana na mgogoro huo; au
 - (ii) mkataba wowote ulio katika maandishi ambao watu wawili au zaidi wamekubaliana kupeleka kwenye usuluishi swali lolote baina yao ambalo limekwisha jitokeza; au
- (b) kuathiri kifungu chochote cha sheria yoyote inayotumika kuhusiana na usuluhishi.

Makubaliano kuwa batili kwa kuto kuwa wazi

29. Makubaliano, ambayo hayako wazi, au ambayo yanaweza yakafanywa yasieleweke, ni batili.

Makubaliano kwa njia ya kuwekeza dau ni batili

30. Makubaliano kwa njia ya kuwekeza dau ni batili; na hakutafunguliwa shauri kwa ajili ya kupata kitu chochote kinachosemekana kilipatikana kutokana na dau lolote, au aliaminiwa mtu yeyote kukubaliana na matokeo ya mchezo wowote au tukio lolote lisilolokuwa na uhakika kwenye dau lolote lilifanywa.

SEHEMU YA IV MIKATABA ISIYO NA UHAKIKA

Tafsiri ya "Mikataba isiyo na uhakika "

31. "Mkataba isiyo na uhakika" ni mkataba wa kufanya au kutofanya kitu, iwapo jambo fulani kuhusiana na mkataba huo litatokea au halitatokea.

Utekelezaji wa mikataba isiyo na uhakika tukio linapotokea

32. Mkataba usio na hakika wa kufanya au kutofanya kitu chochote iwapo kitendo kisichoeleweka cha baadae kikitokea hauwezi kutekelezeka kisheria mpaka pale kitu hicho kitatokea; na kama kitu hakitaweza kutokea basi mkataba huo unakuwa batili.

Utekelezaji wa mikataba isiyo na uhakika tukio lisipotokea

33. Mkataba usio na hakika wa kufanya au kutofanya kitu chochote iwapo tukio lisiloeleweka la baadae halitatokea unaweza kutekelezwa pale tu ikihakikishwa tukio hilo halitokei na sio kabla.

Pale ambapo
mkataba usio
na uhakika
unachukuliwa
kushindikana,
iwapo ni
kitendo
alichopanga
mtu kukifanya
baadae

34. Iwapo tukio la baadae linalohusika na mkataba linategemea tukio la mtu katika muda usiojulikana, tukio litachukuliwa kama lisilowezezekana pale ambapo mtu atafanya hivyo ndani ya muda usiodhaniwa au katika matukio mengine yasiyotarajiwa.

Mkataba usio
na uhakika

35.-(1) Mkataba usio na uhakika wa kufanyika au kutofanyika kwa kwa kutegemea jambo fulani iwapo tukio lisilodhaniwa likatokea katika muda uliopangwa unakuwa batili kama, baada ya muda uliopangwa kuisha tukio hilo halijatokea, au kama, kabla ya muda uliopangwa, tukio limekuwa haliwezekani.

(2) Mkataba usio na uhakika wa kufanyika au kuto fanyika kwa kutegemea jambo fulani iwapo tukio lisilodhaniwa halikutokea katika muda uliopangwa au kabla ya muda uliopangwa kumalizika na tukio halijatokea.

Mkataba usio
wa uhakika
kwa kitu
kisichowezeka
na ni batili

36. Mkataba sio na uhakika wa kufanya au kutofanya kitu chochote, iwapo tukio lisilowezezekana linatokea, ni batili, kama kutokuwezekana kwa tukio kulikuwa kunajulikana au la wahusika katika makubaliano wakati yanafanywa.

SEHEMU YA V UTEKELEZAJI WA MIKATABA

Mikataba ambayo lazima itekelezwe

Wajibu wa
wahusika
katika
mikataba

37.-(1) Wahusika katika mkataba lazima watekeleze ahadi zao, isipokuwa kama utekelezaji umesamehewa chini ya masharti ya sheria hii au sheria nyingine yoyote.

(2) Ahadi zinawafunga wawakilishi wa mtoa ahadi ikitokea mtoa ahadi anafariki kabla ya kutekeleza, isipokuwa kama nia tofauti itajitokeza katika mkataba.

Matokeo ya
kukataa
kupokea
pendekezo la
kutekelezwa

38.-(1) Pale mtoa ahadi amejitoea kutekeleza ahadi kwa mpokea ahadi, na pendekezo halikukubaliwa, mtoa ahadi hahusiki na kutokutekelezwa kwa ahadi, wala hapotezi haki zake chini ya mkataba.

(2) Kila toleo lazima litimize masharti yafuatayo-

- (a) lisiwe na masharti ;
 - (b) lifanyike katika muda na mahali muafaka, na katika mazingira ambayo mtu anayetolewa toleo anaweza kupata wasaa wa kujiridhisha kwamba mtu aliyetoa toleo anaweza na yuko tayari kutekeleza ahadi yake inayomfunga;
 - (c) kama toleo ni toleo la kupeleka kitu chochote kwa mpokeaji, mpokeaji lazima awe na fursa ya kuona kwamba kitu kilichotolewa ni kitu ambacho mtoa ahadi analazimika kupeleka kulingana na ahadi yake.
- (3) Toleo kwa mmoja kati ya wapokeaji wengi lina matokeo sawa ya kisheria kama toleo kwa wote.

Matokeo ya mhusika kukataa kutekeleza ahadi yote

39. Wakati ambapo mhusika katika mkataba amekataa kutekeleza, au kujikwamisha mwenyewe kutekeleza ahadi yake yote, mpokeaji wa ahadi anaweza **kumaliza** mkataba, isipokuwa kama ameonyesha, kwa maneno au vitendo, kuridhia kuendeleza mkataba.

Watu ambao ahadi zinaweza kutekelezwa kwao.

40. Kama itaonekana kulingana na aina ya suala, kwamba ilikuwa nia ya wahusika katika mkataba wowote kuwa ahadi yoyote iliyomo kwenye mkataba lazima itekelezwe na mtoa ahadi mwenyewe, ahadi hiyo lazima itekelezwe na mtoaji, na katika mazingira mengine mtoa ahadi au wawakilishi wake wanaweza kumtumia mtu anayefaa kutekeleza ahadi ile.

Matokeo ya kukubali utekelezaji wa mtu wa tatu

41. Pale mpokeaji anakubali kutekelezwa kwa ahadi na mtu wa tatu, hawezi baadae kulazimisha utekelezaji wake dhidi ya mtoa ahadi.

Madeni na haki za pamoja

Kuhamisha kwa madeni ya pamoja

42. Pale ambapo watu wawili au zaidi wameweka ahadi ya pamoja, basi, isipokuwa tu kama nia tofauti itaonekana katika mkataba, watu hao wote katika maisha yao, na baada ya kifo cha mmoja kati ya hao, mwakilishi wake pamoja na waliobakia, na baada ya kifo cha mtu wa mwisho katika umoja ule, wawakilishi wa wahusika wote lazima watimize ahadi.

Majukumu na madenia ya watoa ahadi wa pamoja

43.-(1) Pale ambapo watu wawili au zaidi wameweka nia ya pamoja, mpokeaji ahadi anaweza kumlazimisha mmoja wa watoa ahadi au wote kutekeleza ahadi yote kama hakuna makubaliano tofauti:

Isipokuwa kwamba kama mpokeaji anaanzisha shauri dhidi ya mmoja au baadhi ya watoa ahadi na akapata ushindi, hakuna kitu katika kifungu kidogo hiki kitahebiwa kuruhusu mpokeaji huyo kufungua shauri lingine linalofanana dhidi ya watoa ahadi waliobaki.

(2) Kila watoa ahadi wawili au zaidi wanaweza kumlazimisha mtoa

ahadi mwingine kwenye kundi kutoa mchango sawa katika kutekeleza ahadi, isipokuwa kama nia tofauti imejitokeza kwenye mkataba.

(3) Ikiwa mmoja kati ya watoa ahadi wawili au zaidi atakuwa amezembea katika kutekeleza ahadi, watoa ahadi waliobaki watafidia pengo lililojitokeza kwa usawa

(4) Hakuna kitu katika kifungu hiki kitamzuia mdhamini kurudishiwa malipo makubwa aliyofanya kwa niaba ya mhusika mkuu, au kumpa haki mhusika mkuu kurudishiwa malipo aliyoyafanya kwa mdhamini kwa malipo yaliyofanywa na mhusika mkuu.

Matokeo ya kumuachilia mmoja kati ya watoa ahadi

44. Pale ambapo watu wawili au zaidi wametoa ahadi ya pamoja, kuachiliwa kwa mtoa ahadi mmoja kunakofanywa na mpokeaji hokusababishi kuachiliwa kwa mtoa au watoa ahadi wengine: wala hakumpi uhuru mtoa ahadi aliyeachiwa dhidi ya wajibu wake kwa watoa ahadi wengine.

Kuhamisha kwa haki za pamoja

45. Pale ambapo mtu anatoa ahadi kwa watu wawili au zaidi kwa pamoja, haki ya kudai utekelezaji baina yao, utakuwa upande wao waliopokea, kwa muda watakao kuwa wanaishi, na baada ya kifo cha mmoja wao, kwa mwakilishi wa marehemu pamoja na mpokea au wapokea ahadi waliobakia, na baada ya kifo cha mpokea ahadi wa mwisho, haki ya kudai utekelezaji inakuwa ya wawakilishi kwa pamoja, labda tu kama mkataba umeelekeza tofauti.

Muda na Mahali pa Utekelezaji

Muda wa kutekeleza ahadi ikiwa hakuna maombi yaliyotolewa na muda haujapangwa

46. Pale ambapo kwa kupitia mkataba, mtoa ahadi anatakiwa kutimiza ahadi yake bila maombi ya mpokeaji, na muda wa kutekeleza haujatajwa, ahadi lazima itekelezwa ndani ya muda wa kawaida, ambao katika hali ya kawaida **inategemea na vitu vinavyihusika.**

Muda na mahala pa kutekeleza ahadi ikiwa muda umepangwa na hakuna maombi kufanywa

47. Wakati ambapo ahadi inatakiwa itekelezwe katika siku fulani, na mtoa ahadi ameamua kutekeleza bila ya maombi ya mpokeaji, mtoa ahadi anaweza kutekeleza katika muda wa kawaida wa kazi katika siku hiyo na mahali ambapo utekelezaji ulitegemewa kufanyika.

Maombi ya kutekeleza

48.-(1) Pale ambapo ahadi inatakiwa itekelezwe siku fulani, na mtoa ahadi hajapanga kutekeleza bila ya maombi ya mpokeaji, ni jukumu la

ahadi kwa
baadhi ya siku
yawe na muda
na mahali
muafaka

mpokeaji kuomba utekelezaji wake akiwa mahali muafaka na ndani ya muda wa kawaida wa kazi.

(2) Swali kwamba mahali na muda muafaka ni upi, inategemea mambo muhimu katika kila shauri.

Mahali pa
kutekeleza
ahadi ikiwa
maombi
hayajatolewa
na hakuna
makubaliano
ya mahali pa
utekelezaji

49. Wakati ambapo ahadi ni ya kutekelezwa bila ya maombi ya mpokeaji, na hakuna mahali maalumu pameandaliwa kwa utekelezaji wake, ni wajibu wa mtoa ahadi kumuomba mpokeaji kutaja mahali pa kutekeleza ahadi, na kutekeleza mahali pale.

Utekelezaji
kwa namna au
kwa muda
ulioelekezwa
au kuwekwa
na mtoa ahadi

50. Utekelezaji wa ahadi yoyote unaweza kufanywa kwa namna yoyote, au kwa wakati wowote atakaoeleza au anaouweka mpokeaji.

Utekelezaji wa Ahadi kwa pamoja

Mtoa ahadi
halazimishwi
kutekeleza
isipokuwa tu
kama mtoa
ahadi mwenz
yupo tayari na
ana nia ya
kutekeleza

51. Kama mkataba una ahadi zinazotakiwa zitekelezwe kwa pamoja, mtoa ahadi hatakiwi kutekeleza hadi mpokeaji awe tayari na awe na nia ya kutekeleza sehemu yake.

Amri ya
kutekeleza
ahadi za
pamoja

52. Pale ambapo amri ya kutekeleza ahadi za pamoja imewekwa bayana kwenye mkataba, ahadi hizo zinabidi zitekelezwe kwa mpangilio huo, na, pale amri haikuelezwa bayana kwenye mkataba, wahusika watatekeleza kwa mpangilio huo kulingana na aina ya shughuli.

Madeni ya
mhusika
anayezuia
tukio ambalo

53. Pale mkataba unapokuwa na ahadi za pamoja, na mhusika mmoja anamzuia mwingine kutekeleza ahadi zake, mkataba unakuwa mkataba unaoweza kubatilika kwa hiari ya mhusika aliyezuiwa; na anastaili kulipwa fidia kutoka kwa mhusika mwingine kwa hasara zozote ambazo anaweza kuwa

lingewezesha
mkataba
kutekelezeka

amepata zinazotokana na kutokutekelezwa kwa mkataba.

Matokeo ya
kushindwa
kutekeleza
ahadi ambayo
ilitakiwa
itekelezwe
kwanza katika
ahadi za
pamoja

54. Pale mkataba unapokuwa na ahadi za pamoja, kiasi kwamba moja kati yao haziwezi kutekelezwa, au kwamba utekelezaji wake hauwezi kudaiwa mpaka mwingine atekeleze, na mtoa ahadi aliyetajwa wa mwisho akishindwa kutekeleza, mtoa ahadi huyo hawezi kudai utekelezaji wa pamoja, na anatakiwa atoe fidia kwa mhusika mwenzake kwa hasara yoyote atakayokuwa ameisababisha kwa mhusika mwenzake kwa kutotekeleza ahadi yake.

Matokeo ya
kushindwa
kutekeleza
kwa wakati
ulioyekwa
katika
mkataba

55.-(1) Pale ambapo mhusika katika mkataba ameahidi kufanya kitu fulani kwa wakati fulani au kabla ya muda fulani, au vitu Fulani kabla ya muda, na akashindwa kufanya chochote kati ya alivyoahidi kabla au katika muda uliotajwa, mkataba huo, unakuwa mkataba unaoweza kubatilika kwa hiari ya mpokea ahadi, kama madhumuni ya wahusika yalilenga muda kuwa ni kitu muhimu kwenye mkataba.

(2) Iwapo haikuwa kusudio la wahusika kwamba suala la muda ni muhimu katika mkataba, mkataba hauwezi kuwa mkataba unaoweza kubatilika kwa kushindikana kufanyika wakati au kabla ya muda uliopangwa; lakini mpokea ahadi anastahili fidia kutoka kwa mtoa ahadi kwa hasara yoyote itakayojitokeza kwa kushindikana huko.

(3) Iwapo katika suala la mkataba unaoweza kubatilika uliosababishwa na mtoa ahadi kushindwa kutekeleza ahadi katika muda uliokubalika, mpokeaji ahadi akakubali kutekelezwa kwa ahadi katika muda tofauti na uliokubalika, mpokeaji hawezi kudai fidia kwa hasara yoyote itakayotokana na kutokutekelezwa kwa ahadi katika muda uliokubalika, isipokuwa tu kama wakati wa kukubali utekelezaji alitoa taarifa kwa mtoa ahadi.

Makubaliano
ya kufanya
kitendo
kisichowezeka
na, chenye
ugumu au
kisicho halali
na fidia husika

56.-(1) Makubaliano ya kufanya kitu kisichowezekana ni batili.

(2) Mkataba wa kufanya kitu ambacho, baada ya mkataba kukamilika kinakuwa hakiwezekani, au kwa sababu ya tukio fulani ambalo mtoa ahadi hakuweza kulizuia, usio halali, unakuwa ni batili ikiwa kitendo kile kinakuwa hakiwezekani au si halali.

(3) Pale ambapo mtu mmoja anaahidi kufanya kitu ambacho anajua, au katika hali ya kawaida alitakiwa kujua, na ambayo mpokea habari hakuajua kuwa kitu hicho hakiwezekani au ni kinyume na sheria, mtoa ahadi huyo anatakiwa alipe fidia kwa mhusika kwa hasara yoyote atakayoipata kwa kushindikana kutekelezeka kwa ahadi hiyo.

Ahadi za
pamoja za
kufanya vitu
halali, na pia
vitu vingine
visivyo halali

57. Pale ambapo watu wanatoa ahadi kwa pamoja, kwanza kufanya vitu fulani halali na pili, katika mazingira fulani, kufanya vitu fulani ambavyo si halali, fungu la kwanza la ahadi ni mkataba, lakini fungu la pili ni makubaliano yanayoweza kubatilika.

Ahadi
mbadala
mojawapo
kuwa si halali

58. Katika suala la ahadi mbadala, tawi mojawapo ikiwa ni halali na lingine sio halali, lile tawi halali ndio litakalotekelezwa.

Kujitengea Malipo

Maombi ya
malipo ikiwa
deni
linalotakiwa
kulipwa
limeonyeshwa

59. Pale ambapo mdaiwa mwenye madeni mengi kwa mtu mmoja, anamlipa kwa makubaliano fulani au katika mazingira kwamba malipo yatumike kulipia deni fulani, malipo hayo yakikubalika, yanatakiwa yatumike ipasavyo.

Maombi ya
malipo ikiwa
deni
linalotakiwa
kulipwa
halijaonyeshwa

60. Pale ambapo mdaiwa anashindwa kuwa muwazi, na hakuna mazingira yanayoonyesha malipo hayo ni kwa deni lipi, mlipwaji anaweza kutumia malipo hayo kwa deni lolote halali lililotakiwa kulipwa, kama ulipaji wake unazuiwa na sheria yeyote inayotumika au la kuhusiana na ukomo wa kuanzisha mashauri.

Maombi ya
malipo ikiwa
hakuna
mhusika
aliyejitengea
malipo

61. Pale ambapo hakuna mhusika yeyote anayejitengea malipo, malipo yatatumika kulipia madeni kulingana na muda wa madeni hayo yalivyopatikana, bila kujali kama yana ukomo wowote wa kisheria au la; na kama madeni yanalingana, malipo yatatumika kulipia madeni yote kwa uwiano.

Mikataba Ambayo Haitakiwi Kutekelezwa

Matokeo ya
kuhuishwa,
kubatilishwa
na
kubadilishwa
kwa mkataba

62. Iwapo wahusika katika mkataba wamekubaliana kubadilisha mkataba mpya kwa wa zamani, kuufuta au kubadilisha yaliyomo, mkataba wa awali hautakiwi kutekelezwa.

Mpokea ahadi
anaoweza
kuacha ama
kutekeleza
ahadi

63. Kila mpokea ahadi anaweza kuacha kutekeleza ahadi yote au sehemu ya ahadi, au anaweza kukubali, akiridhika, kitu chochote badala ya kutekeleza mkataba kama atakavyoona inafaa.

Matokeo ya
kubatilisha
mkataba
unaoweza
kubatilika

64. Wakati ambapo mtu ambaye kwa hiari yake mkataba unaweza kubatilika amejitoa, mhusika mwingine hawezi kutekeleza ahadi yoyote kwenye mkataba ule ambaye yeye ni mtoa ahadi; na mhusika aliyejitoa kwenye mkataba, anatakiwa, kama amejipatia faida yoyote kutoka kwa mhusika mwingine, kuhuisha faida hiyo kwa mtu aliyejitatia faida hiyo,atarudisha faida hiyo kwa kiasi kile, kwa mtu yule aliyetoa.

Wajibu wa
mtu
aliyenufaika
kwa mkataba
batili au
mkataba
unaoweza
kubatilika

65. Wakati ambapo makubaliano yanagundulika kuwa ni batili, au mkataba unapoweza kubatilika, mtu yeyote aliyenufaika na makubaliano au mkataba huo anatakiwa kurudisha kulipa fidia kwa mhusika ambaye amesababisha kupatikana kwa manufaa hayo:

Isipokuwa kwamba pale ambapo mkataba ni kuwa batili kwa sababu zilizopo kwenye kifungu kidogo cha (2) cha kifungu cha 56, na mhusika akaingia gharama kabla ya mkataba kutekelezwa au kwa ajili ya kutekeleza mkataba huo, mahakama inaweza, kama itaona inafaa kulingana na mazingira ya kesi, kumkubalia mtu huyo kubaki na sehemu ya manufaa hayo au kubaki na manufaa yote, au kumtaka mtu huyo kulipa fidia, au kutoa amri kwamba mtu huyo arudishe manufaa yote aliyoyapata au sehemu ya manufaa hayo au malipo ambayo angeyapata kama mkataba usingekuwa batili, ikiwa manufaa au malipo siyo makubwa zaidi ya gharama aliyoingia.

Jinsi ya kutoa
taarifa juu ya
kufuta,
ubatilishaji wa
mkataba
unaoweza
kuwa batili

66. Taarifa ya ubatilishaji au ufutwaji wa mkataba unaoweza kufanywa kwa namna ileile na kwa kanuni na kufuatana na kanuni zile zile zinazotumika kwenye kutaarifu au kufuta pendekezo yanavyofanyika.

Matokeo ya
uzembe wa
mpokea ahadi

67. Iwapo mpokea ahadi yeyote anazembea au anakataa kumpatia mtoa ahadi vitendea kazi vizuri vitakavyosaidia kutimiza ahadi yake, kutokana na uzembe huo mtoa ahadi anasamehewa kwa kushindwa kutekeleza kunakosababishwa na kukosekana kwa vitendea kazi.

SEHEMU YA VI MAHUSIANO YANAYOFANANA NA YALE YALIYOTOKANA NA MKATABA

Madai
muhimu ya

68. Iwapo mtu hawezi kuingia mkataba, au mtu yeyote ambaye kisheria anatakiwa kusaidia anapatiwa na mtu mwingine vitu muhimu katika maisha,

huduma aliyopewa mtu asiyestahili kuingia mkataba au kwa jili yake mwenyewe mtu ambaye ametoa vitu hivyo anatakiwa kurudishiwa kutoka kwenye mali za yule asiyeweza kuingia mkataba.

Marejesho ya pesa kwa aliyelipa ikiwa ni malipo yenye manufaa kwake **69.** Mtu mwenye kupenda kulipa pesa ambayo mtu mwingine analazimika kisheria kulipa, na akalipa, anatakiwa kurejeshewa na mhusika huyo mwingine.

Wajibu wa mtu aliyefurahia manufaa ya vitendo ambavyo si vya bure **70.** Pale ambapo mtu anafanya kitu halali kwa mtu mwingine , au kumpa kitu, bila kuonyesha ulazima fulani na mtu huyo aliyepokea akafurahia, mpokeaji anatakiwa kulipa fidia kwa mtoaji wa kitu au huduma huyo:

Isipokuwa kwamba hakuna fidia itakayotolewa ikiwa anayetakiwa kutoa fidia hakuwa na nafasi ya kukubali au kukataa.

Majukumu ya aliyefichua mali **71.** Mtu ambaye amefichua mali ya mtu mwingine, na akiweka chini ya himaya yake, anakuwa na jukumu sawa na mdhaminiwa.

Deni la mtu ambaye pesa au mzigo vimelipwa kwake kwa makosa au kwa lazima **72.** Mtu ambaye amelipwa pesa, au kitu kimetumwa kwake kwa makosa, kama ikithibitika kuwa itasababisha jukumu la kisheria, lazima alipe au arudishe.

SEHEMU YA VII MATOKEO YA KUVUNJA MKATABA

Fidia kwa hasara au uharibifu uliosababishwa na **73.-(1)** Wakati ambapo mkataba unakuwa umevunjika, mhusika ambaye ameathirika na ukiukaji huo anastahili kupata fidia ya hasara iliyojitokeza kutoka kwa aliyesababisha ukiukwaji wa mkataba huo, au fidia iliyosababishwa na kujitokeza kwa mambo fulani ambayo ni ya kawaida katika uvunjaji wa mkataba, au ambayo wahusika walijua walipofanya mkataba

kuvunjika kwa walijua yaweza kutokea iwapo mkataba utavunjwa..
mkataba

(2) Fidia haitakiwi kutolewa kwa hasara ambayo imejificha au siyo ya moja kwa moja.

(3) Wakati kunapotokea majukumu yanayofanana na yale yaliyomo kwenye mkataba na yakawa hayajatekelezwa, mtu yeyote atakayeathirika na kutotekelezwa huko anastahili kupata fidia ileile kutoka kwa mhusika aliyesababisha kama vile mtu huyo aliingia mkataba wa kutekeleza na kushindwa kufanya hivyo.

(4) Katika kukadiria hasara au uharibifu uliotokana na kuvunjwa kwa mkataba, utaratibu au njia za kufidia madhara yaliyosababishwa kama vile mtu huyo aliingia mkataba wa kuutekeleza na akavunja mkataba.

Fidia kwa kuvunjika kwa mkataba pale ambapo adhabu inajulikana

74.-(1) Wakati ambapo mkataba unapokuwa umevunjika, kama kiwango cha fedha kimetajwa kwenye mkataba kuwa ndio malipo yatakayofanywa kwa kuvunjwa kwa mkataba, au kama mkataba umeelekeza adhabu nyingine yoyote, mhusika anayelalamika kuhusu uvunjaji huo unastahili kutoka kwa mhusika mwingine aliyevunja mkataba, fidia inayoeleweka isiyozidi kiwango kilichotajwa au kama itakavyokuwa, adhabu iliyowekwa.

(2) Masharti kwamba faida itaongezeka kuanzia tarehe ya ushindwa kutekeleza mkataba yanaweza kuwa kwa njia ya adhabu.

(3) Bila kujali masharti ya vifungu vilivyotangulia katika kifungu hiki, ikitokea mtu yeyote anaingia kwenye udhamini, ahadi ya mahakama au ahadi nyingine ya aina hiyo au kwa amri ya Serikali au Rais wa nchi anaweza ahadi ya kutekeleza ahadi ya shughuli za jamii au kitendo ambacho jamii itanufaika, atakuwa amekosea kama amekiuka masharti ya chombo hicho na kutakiwa kulipa kama ilivyo katika mkataba.

(4) Ili kuondoa shaka, inaelezwa kwamba mtu anayeingia mkataba na Serikali au na Rais wa nchi sio lazima awe amefanya kazi yoyote ya umma, au ametoa ahadi ya kufanya kitu chenye manufaa kwa umma.

Mhusika anayebatilisha mkataba kwa haki unastahili fidia

75. Mtu ambaye ameamua kubatilisha kwa haki mkataba anastahili kupata fidia kwa madhara aliyoyapata kwa kutotekeleza mkataba.

SEHEMU YA VIII FIDIA BIMA NA DHAMANA

Tafsiri ya "Mkataba wa Fidia Bima "

76. Mkataba ambao mhusika mmoja anaahidi kumuokoa mwingine asipate hasara aliyosababisha unaitwa "mkataba wa fidia-bima".

Haki za

77. Mtoa ahadi katika mkataba wa fidia-bima, akifanya chochote ndani

mwenye fidia ya mamlaka yake, anastahili kurudishiwa na mtoa ahadi-
bima-
akishitakiwa
n.k

- (a) madhara yote ambayo anaweza kulazimishwa kulipa katika shauri lolote la mahakama ambalo ahadi ya fidia bima imetumika;
- (b) gharama zote ambazo anaweza kulazimishwa kuzilipa katika mwenendo wowote kama, katika kulipa gharama au kuzitetea hajakiuka amri ya mtoa ahadi, na kufanya kitendo hicho kama busara kwake kwa kutenda bila ya kuwepo kwa mkataba wa fidia bima, au kama mtoa ahadi alimruhusu kuanzisha au kulipia shauri hilo; na
- (c) gharama zote ambazo anaweza kuwa amezitumia kulipia mahakamani kwa makubaliano, kama makubaliano hayapingani na ahadi za mtoa ahadi, na malipo ambayo yalikuwa lazima yafanyike hata bila makubaliano au kama mtoa ahadi alimruhusu kufanya malipo hayo.

Tafsiri ya
"Mkataba wa
mdhamini
"mdhamini
"mdaiwa
mkuu", na
"mkopeshaji"

78. "Mkataba wa udhamini" ni mkataba wa kutekeleza ahadi, au kutekeleza majukumu ya mtu wa tatu ikitokea ameshindwa kutekeleza na mtu anayetoa udhamini anaitwa mdhamini; mtu ambaye akishindwa kutekeleza dhamana imetolewa anaitwa mdaiwa mkuu, na mtu ambaye dhamana imetolewa kwake anaitwa mkopeshaji; na dhamana inaweza kuwa ya maandishi au ya maneno.

Malipo ya
udhamani

79. Kitu chochote kinachofanyika, au ahadi yoyote inayotolewa kwa manufaa ya mdaiwa mkuu kinaweza kuwa ni malipo yanayojitosheleza kwa mdhamini kutoa dhamana.

Deni la
mdhamini

80. Majukumu ya mdhaminiwa yanaenda sambamba na ya mdhamini, isipokuwa tu kama imetajwa vinginevyo kwenye mkataba.

Tafsiri ya
"Dhamana
endelevu "

81. Dhamana inayohusisha mlolongo wa matukio inaitwa "dhamana endelevu".

Kufutwa kwa
dhamana
endelevu

82. Dhamana endelevu inaweza ikafutwa wakati wowote na mdhamini kwaajili ya shughuli ya baadae kwa kutoa taarifa kwa mdhaminiwa.

Kufutwa kwa
dhamana
endelevu
kutokana na
kifo cha

83. Kifo cha mdhamini, ikiwa mkataba haujaelekeza vinginevyo, kinatumika kama sitisho la kutekeleza ahadi ya baadae, kuhusiana na ahadi za baadae.

mdhamini

Deni la watu
wawili, wenye
deni la msingi,
halitaathriwa
na mipango
yao kwamba
mmoja
atakuwa
mdhamini
dhidi ya
mwingine

84. Pale ambapo watu wawili wanafanya mkataba na mtu wa tatu kwaajili ya kutekeleza kitu fulani, na pia kuingia mkataba baina yao, kila mmoja wao atakuwa na hatia kwa uzembe wa mwingine, mtu wa tatu akiwa si sehemu ya mkataba huo, hatia kwa kila mtu kati ya wale wawili kuhusiana na mtu wa tatu kuhusiana na mkataba wa kwanza haivurugwi kwa kuwepo kwa mkataba wa pili, ingawa mtu huyo watatu anaweza kuwa na ufahamu wa kuwepo kwa mkataba huo.

Kuachwa kwa
mdhamini
kutokana na
kubadilika
kwa masharti
ya mkataba

85. Mabadiliko yoyote yanayofanywa bila ridhaa ya mdhamini kuhusiana na masharti ya mkataba kati ya mdaiwa mkuu na kopeshaji, hayamhusu mdhamini kutekeleza zaidi ya makubaliano na kuacha mabadiliko.

Kuachiwa kwa
mdhamini
kutokana na
kuachiwa kwa
mdaiwa mkuu

86. Mdhamini hahusiki na mkataba baina ya mkopeshaji na mdaiwa mkuu ambapo mdaiwa mkuu ameachiwa au kwa kutofanya au kufanya kitu fulani kwa mkopeshaji, ambacho matokeo yake ni kuachiwa kwa mdaiwa mkuu.

Kuachiwa kwa
mdhamini
wakati
mkopeshaji
atakapojipa
muda, na
kuamua kuto
kumshitaki
mdaiwa mkuu

87. Mkataba baina ya mkopeshaji na mdaiwa mkuu, ambao mkopeshaji anajitolea au anatoa ahadi ya kuongeza muda, wa kumshtaki mdaiwa mkuu, mkataba unamuacha mdhamini isipokuwa kama mdhamini ameukubali mkataba huo.

Mdhamini
haachiwi kama
makubaliano
yamefanywa
na mtu
mwingine na
kumpa muda
mdaiwa mkuu

88. Pale mtu wa tatu, na wala sio mdaiwa mkuu, anapoandaa mkataba wa kumuongezea muda mdaiwa, mkuu mdhamini hataachiwa.

Msamaha wa
mkopeshaji
kufungua
mashitaka
hakumuachi
mdhamini

89. Msamaha wa mkopeshaji kumshitaki mdaiwa mkuu au kudai madai mengine yoyote, bila ya kuwepo kifungu kinachotoa maelezo tofauti, hakuwezi kumwachia mdhamini.

Kuachiwa kwa
mdhamini
mwenz
hakusababishi
wengine
kuachiwa

90. Pale ambapo kuna wadhamini wa pamoja, mdhamini mmoja akiachiwa na mkopeshaji, kutolewa huko hakuwaondoi wengine; na wala hakumuachi mdhamini huyo, kutoka kwenye majukumu yake kwa wadhamini wengine.

Kuachiwa kwa
mdhamini
kunakosababis
hwa na
mkopeshaji
kunapelekea
mdhamini
kupata nafuu

91. Iwapo mkopeshaji anafanya kitendo chochote ambacho ni kinyume na haki ya mdhamini, au ameacha kufanya kitu ambacho alitakiwa na mdhamini kukifanya, na baadae haki ya mdaiwa mkuu ikaondolewa, mdhamini anaachiwa.

Haki za
mdhamini
kuhusu malipo
au
kutekelezwa
kwa mkataba

92. Pale ambapo deni lililodhaminiwa linatakiwa kulipwa, au mdaiwa mkuu amezembea kutimiza kazi zake alizotakiwa kuzifanya, kudhamini, kulipa au kufanya alichotakiwa kukifanya, anakuwa na haki zote ambazo kopeshaji alikuwa nazo dhidi ya mdaiwa mkuu.

Haki ya
mdhamini
kuwanufaisha
wadhamini wa
kopeshaji

93. Mdhamini anastahili manufaa dhidi ya kila mali ambayo mkopeshajianayo dhidi ya mdaiwa mkuu, kama mali hiyo ilikuwepo wakati mkataba wa udhamini unasainiwa au mkataba unakuwepo, na kama mdhamini uwepo wa mali au la, na, kama mkopeshaji anakosa dhamana au, bila ya ridhaa ya mdhamini, anaigawa mali hiyo, dhamana inatekelezwa kulingana na thamani ya mali.

udhamini
unaopatikana
kwa
uwakilishi wa
uongo si halali

94. Udhamini wowote unaopatikana kwa uwakilishi wa uongo unaofanywa na mkopeshaji, au kwa kufahamu na kwa ridhaa yake, kuhusiana na kitu cha msingi kwenye mchakato si halali.

udhamini
unaopatikana

95. Udhamini wowote ambao kopeshaji ameupata kwa kuwa kimya kuhusiana na mazingira muhimu si halali.

kwa mbinu si
halali

dhamana
katika
mkataba
ambao
mkopeshaji
hawezi
kufanya
chochote hadi
wadhamini
wenzwa
wajiunge

96. Pale mtu anapotoa dhamana kwenye mkataba, ambapo mkopeshaji hawezi kufanya chochote hadi mtu mwingine ajiunge kama mdhamini mwenzwa, udhamini huo hawezi kuwa halali kama mtu huyo hajaiunga.

Ahadi ya
kumaanisha ya
kumfidia
mdhamini

97. Katika kila mkataba wa udhamini kuna ahadi ya kumaanisha inayofanywa na mdaiwa mkuu ya kumfidia mdhamini; na mdhamini anastahili kupata kutoka kwa mdaiwa mkuu kiasi halali chochote ambacho amelipa katika udhamini, na sio kiasi alicholipa kwa makosa.

Wadhamini
wenzwa
kupaswa
kulipa sawa

98. Pale ambapo watu wawili au zaidi ni wadhamini wenzwa kwa deni au jukumu linalofanana, iwe kwa pamoja au mmoja mmoja, na kama katika mkataba mmoja au tofauti, na kama wanafahamiana au la, wadhamini wenzwa, bila ya kuwepo kwa mkataba unaoelezea vinginevyo, wanakuwa na hatia, kati yao, kila mmoja kulipa katika uwiano sawa deni lote, au sehemu ya deni ambayo inakuwa haijalipwa na mdaiwa mkuu.

Madeni ya
wadhamini
wenzwa
kufungwa kwa
kiasi tofauti

99. Wadhamini wenzwa ambao wanafungwa kwa kiasi tofauti cha pesa wanatakiwa kulipa sawa kulingana na ukomo wa majukumu yao unavyowaruhusu.

SEHEMU YA IX DHAMANA

Tafsiri ya
"dhamana",
"mdhamini"
na "mdhamini
wa"

100.-(1)"Dhamana" ni kitendo cha mtu kupeleka bidhaa kwa mtu mwingine kwa madhumuni fulani, na kwa kuwepo kwa mkataba kwamba, dhumuni likikamilika, bidhaa vitarudishwa au kuondolewa kulingana na maelekezo ya mtu aliyepeleka vitu vile; na mtu aliyepeleka bidhaa zile anaitwa "mdhamini" wakati mtu ambaye bidhaa zinatolewa kwa ajili yake anaitwa "mdhaminiwa".

(2) Iwapo mtu tayari ana bidhaa za mkataba mwingine ambazo anazo kama mdhaminiwa, kwa maana hiyo anakuwa mdhaminiwa na mtoaji anakuwa mdhamini, wa bidhaa zile zinaweza kuwa hazijatolewa kwa njia ya udhamini.

Jinsi ambavyo mdhaminiwa anapelekewa bidhaa.

101. Kupeleka bidhaa kwa mdhaminiwa kunaweza kutekelezwa kwa kufanya kitu ambacho kina matokeo ya kuweka bidhaa mikononi mwa mdhaminiwa au kwa mtu yeyote mwenye dhamana ya kushika bidhaa hizo kwa niaba yake.

Wajibu wa mdhamini kutoa dosari katika bidhaa zilizodhaminiwa

102.-(1) Mdhamini anatakiwa kuweka wazi kwa mdhaminiwa dosari katika bidhaa zilizowekwa dhamana, ambazo anazifahamu, na ambazo zitaingiliana na matumizi ya bidhaa hizo, au, ambazo zitamfanya mdhaminiwa kuwa katika hatari; na, kama hatoweka wazi, atawajibika kwa madhara ya moja kwa moja yatakatayompata mdhaminiwa kutokana na dosari hizo

(2) Iwapo bidhaa zimewekwa dhamana kwa kukodishwa, mdhamini atawajibika kwa madhara hayo, iwe alikuwa anajua au la, kuhusu kuwepo kwa dosari katika bidhaa aliyoiweka kama dhamana.

Uangalifu anaopaswa kuwa nao mdhaminiwa

103. Katika masuala yote ya udhamini, mdhaminiwa anatakiwa kutunza bidhaa zilizowekwa dhamana kwake, kama mtu yeyote mwenye busara ambavyo angefanya, katika hali kama hiyo, kuchukulia kama bidhaa zingekuwa zake kwa ukubwa, ubora na thamani ya bidhaa zilizowekwa dhamana:

Isipokuwa kwamba hakuna kitu chochote katika kifungu hiki kitachukuliwa kama kutumia au kufananisha kosa katika sheria za mapokeo kwa mtoa huduma wa kawaida au mtunzaji.

Wakati ambapo mdhaminiwa hawajibiki kwa hasara, nk ya kitu kilichowekwa dhamana

104. Mdhaminiwa, bila ya kuwepo kwa mkataba wowote maalum, hawajibiki kwa upotevu, uharibifu au kupotea kwa thamani ya kitu kilichodhaminiwa, kama atakuwa ametunza kama ilivyoelekezwa katika kifungu cha 103.

Kusitishwa kwa dhamana kutokana na matendo ya mdhaminiwa kinyume na masharti

105. Mkataba wa udhamini ni mkataba unaoweza kubatilika kwa hiari ya mdhamini, kama mdhaminiwa akifanya kitendo chochote kuhusiana na bidhaa iliyowekwa dhamana, kinyume na masharti ya udhamini.

Wajibu wa mdhaminiwa aliyeruhusu matumizi ya

106. Iwapo mdhaminiwa anatumia bidhaa yoyote iliyowekwa dhamana, kinyume na masharti ya dhamana, ana wajibu wa kumlipa fidia mdhamini kwa madhara yoyote yaliyojiokeza kutokana na kutumia bidhaa hiyo.

mali
zilizowekwa
dhamana

Matokeo ya
mchanganyiko
, kwa ridhaa
ya mdhamini
juu ya bidhaa
zake na za
mdhaminiwa

107. Iwapo mdhaminiwa, kwa ridhaa ya mdhamini, anachanganya bidhaa za mdhamini na za kwake, mdhamini na mdhaminiwa watakuwa na manufaa kwa uwiano na kulingana na sehemu za michango yao, katika mchanganyiko uliojitokeza.

Matokeo ya
mchanganyiko
, bila ya ridhaa
ya mdhamini
ikiwa mali
zinaweza
kuchanganuli
wa

108. Iwapo hakuna ridhaa ya mdhamini, mdhaminiwa anachanganya bidhaa za mdhamini na zake, na bidhaa zinaweza kuchanganuliwa, umiliki wa bidhaa utabakia kwa wahusika ipasavyo; lakini mdhaminiwa anatakiwa kugharamia uchanganuliwaji utakaofanywa na madhara yoyote yatakoyojitokeza katika mchanganyiko huo.

Matokeo ya
mchanganyiko
, bila ya ridhaa
ya mdhamini
ikiwa bidhaa
haziwezi
kuchanganuli
wa

109. Iwapo hakuna ridhaa ya mdhamini, mdhaminiwa anachanganya bidhaa zake na mdhamini, kiasi kwamba bidhaa haziwezi kuchanganuliwa kati ya zilizowekwa dhamana na nyinginezo na kuzirudisha, mdhamini anastahili kulipwa na mdhaminiwa thamani ya bidhaa zilizopotea.

Malipo ya
gharama za
lazima
afanyayo
mdhamini

110. Pale ambapo, kulingana na masharti ya udhamini, bidhaa zinatakiwa ziwewe au zichukuliwe, au zifanyiwe kitu fulani na mdhaminiwa kwa faida ya mdhamini, na mdhaminiwa hastahili ujira wowote, mdhamini atamlipa mdhaminiwa gharama muhimu alizoziingia kwa madhumuni ya udhamini huo.

Kurudishwa
kwa bidhaa
zilizoazimwa
bila malipo

111. Mtu anayeazimisha kitu kwa ajili ya matumizi, anaweza kudai kirudishwe wakati wowote, kama alitoa bure, hata kama alitoa kwa muda au shughuli maalumu; lakini, kama, katika hali ya kawaida mkopo huo uliofanywa kwa muda na shughuli maalum, mkopaji amefanya kitendo ambacho urudishaji wa kitu kilichotolewa kabla ya muda waliokubaliana utamsababishia kupata hasara zaidi ya faida aliyoipata kutokana na mkopo huo, mtoaji, kama atalazimisha kurudishwa kwa mali, atamfidia mkopaji kiwango ambacho kilizidi faidi aliyoitoa.

Kurudishwa

112. Ni wajibu wa mdhaminiwa kurudisha au kutoa mali

kwa mali
zilizowekwa
dhamana
muda wake
unapokwishaa
u madhumuni
yake kutimia

zilizodhaminiwa kulingana na maelekezo aliyoyatoa mdhamini, bila ya kudaiwa mara muda waliokubaliana unapotimia, au madhumuni ya udhamini huo yanapotimia.

Wajibu wa
mdhaminiwa
ikiwa bidhaa
hazijarudishwa

113. Iwapo kwa makosa ya mdhaminiwa, bidhaa hazirudishwi au kutolewa katika muda uliokubaliwa, atawajibika kwa mdhamini kwa hasara yoyote, uharibifu au uchakavu wa mali kuanzia wakati huo.

Kukatishwa
kwa dhamana
isiyo na
malipo kwa
kifo

114. Dhamana ya bure inasitishwa kwa kifo cha mmoja kati ya mdhamini au mdhaminiwa.

Mdhaminiwa
anatakiwa
kuongeza au
kunufaisha
mali
iliyowekwa
dhamana

115. Bila ya kuwepo kwa mkataba wowote kinyume na haya, mdhaminiwa anatakiwa kutoa kwa mdhamini, au kulingana na maelekezo, nyongeza yoyote au faida ambayo anaweza kuwa ameipata kutoka kwa mali iliyotolewa.

Wajibu wa
mdhamini kwa
mdhaminiwa

116. Mdhamini anawajibika kwa mdhaminiwa kwa hasara yoyote ambayo mdhaminiwa anaweza kuipata kwa sababu tu mdhamini hakutakiwa kutengeneza udhamini, au kupata marejesho ya bidhaa, au kutoa maelekezo kuhusiana nazo.

Dhamana ya
wadhamini
wenza

117. Iwapo wamiliki kadhaa wa bidhaa wameziweka dhamana, mdhaminiwa anaweza kurudisha, au kulingana na maelekezo ya mmiliki mmoja bila ya ridhaa ya wengine, bila ya kuwepo kwa makubaliano mengine yoyote kinyume chake.

Mdhaminiwa
hawajibiki
kwa mdhamini
hewa

118. Iwapo mdhamini hana umiliki wa bidhaa na mdhaminiwa, kwa nia njema, anazirudisha, au kulingana na maelekezo ya, mdhamini, hawajibiki kwa mmiliki wa bidhaa katika kurejesha huko.

Haki ya mtu
wa tatu
anayedai
bidhaa

119. Iwapo mtu, mbali na mdhamini, anadai bidhaa zilizowekwa dhamana anaweza kuomba mahakamani kuzuia urudishwaji wa bidhaa kwa mdhamini, na kuamua milki ya bidhaa hizo.

zilizowekwa
dhamana

Haki ya
aliyefichua
bidhaa

120. Mtu liyefichua bidhaa hana haki ya kudai fidia kwa mmiliki kwa matatizo au gharama alizoziingia kwa hiari yake katika kutunza na kumtafuta mwenye bidhaa; lakini anaweza kubaki na bidhaa hadi atakapopata fidia; na, kama mmiliki ametangaza zawadi maalum kwa atakayerudisha bidhaa, mtafutaji anaweza kushitaki ili apate zawadi hiyo, na anaweza kubaki na bidhaa hiyo hadi atakapopatiwa zawadi

Wakati
ambapo
aliyefichua
bidhaa
inayouzika
anapoweza
kuiuza

121. Wakati ambapo kitu kilichokuwa kiuzwe kimepotea, kama katika hali ya kawaida mmiliki hawezi kupatikana, au kama akikataa kulipia gharama kwa aliyefichua akitakiwa kufanya hivyo, aliyefichua anaweza kuuza-

- (a) kama kitu kina hatari ya kuoza au kupoteza sehemu kubwa ya thamani yake; au
- (b) kama gharama halisi ya aliyekifichua, kuhusiana na kitu kilichofichuliwa, inafikia thamani ya sehemu ya mbili ya tatu ya kitu hicho.

Wakati
ambapo deni
la mshika
bidhaa za
rehani
litakapolipwa

122. Wakati ambapoa mdhaminiwa, kulingana na dhumuni la dhamana, ametoa huduma yoyote iliyohitaji nguvu au uwezo fulani kuhusiana na bidhaa iliyowekwa dhamana, bila ya kuwepo mkataba mwingine, ana haki ya kubaki na bidhaa hizo hadi atakapolipwa ujira kulingana na huduma aliyoitoa kuhusiana na bidhaa husika.

Wakati
mtumishi wa
benki
anaposhikilia
bidhaa kama
rehani

123. Watumishi wa mabanki, mawakili, madalali na watu wengine kama hao, mbali na mikataba mingine, kwa ajili ya usalama wa mahesabu, watabaki na bidhaa yoyote iliyowekwa dhamana kwao; lakini mtu mwingine yeyote hana haki ya kufanya hivyo isipokuwa kama kuna mkataba kwa ajili hiyo.

Dhamana ya ahadi

Tafsiri ya
"ahadi", "mtoa
rehani", na
"muweka
rehani"

124. Dhamana ya bidhaa kama kigezo cha kulipa deni au kutekeleza ahadi inaitwa "ahadi"; na mdhamini katika suala hili anaitwa "mtoa ahadi" wakati mdhaminiwa anaitwa "muweka rehani".

Haki ya kushikilia bidhaa ya muweka rehani

125. Muweka rehani anaweza kushikilia bidhaa iliyowekwa rehani, sio tu kwa ajili ya malipo ya deni au kutekeleza ahadi, lakini pia kwa ajili ya faida iliyojaliwa na deni na gharama zingine alizoziingia kuhusiana na kushikilia zile bidhaa zilizowekwa rehani.

Muweka rehani kutoshikilia kwa ajili ya deni au ahadi zaidi ya zile zilizowekewa ahadi

126. Kama hakuna mkataba, muweka rehani hawezi kubaki na bidhaa zilizowekwa rehani kutokana na deni au ahadi zingine tofauti na deni au ahadi iliyokusudiwa; lakini mkataba huo unaweza kufikiriwa kutokana na maombi yatakayotolewa na muweka rehani.

Dhana ya maombi ya nyongeza

Haki ya kuweka rehani ikiwa atakosea

Haki ya mtoa rehani ikiwa kuna gharama za nyongeza

127. Muweka rehani anastahili kulipwa gharama za nyongeza alizoziingia kwa ajili ya kutunza bidhaa zilizowekwa rehani kutoka kwa aliyetoa bidhaa zilizoahidiwa.

Haki ya muweka rehani ikiwa atakosea

128.-(1) Iwapo mtoa rehani atachelewa kulipa deni au kutekeleza ahadi katika muda uliokubalika, na ni ahadi ambayo ilisababisha bidhaa kuwekwa rehani, muweka rehani anaweza kuanzisha shauri dhidi ya mtoa rehani, na akabaki na bidhaa zilizowekwa rehani kama dhamana yake; au anaweza kuuza bidhaai zilizowekwa rehani kwa kumpa mtoa rehani taarifa ya muda wa kutosha kufanya hivyo.

(2) Iwapo mapato ya mauzo hayo ni pungufu ya pesa inayodaiwa iliyoahidiwa, mtoa rehani bado anatakiwa kulipa tofauti iliyojitokeza lakini kama mapato ya mauzo ni makubwa kuliko deni, muweka rehani atarudisha ziada kwa mtoa rehani.

Haki ya kudai ya muweka rehani aliyekosea

129. Iwapo muda umepangwa kwa ajili ya kulipa deni au kutekeleza ahadi, ambapo bidhaa imewekwa rehani, na mtoa rehani ameshindwa kulipa deni au kutekeleza wajibu wake katika muda uliokubalika, anaweza kudai bidhaa zilizowekwa rehani wakati wowote kabla hazijauzwa; lakini anatakiwa kulipa gharama zozote zilizojitokeza kutokana na kuchelewa kwake kulipa.

Ahadi ya wakala wa biashara na

130.-(1) Pale ambapo, kwa ridhaa ya mmiliki, wakala wa biashara ameshikilia bidhaa au nyaraka za bidhaa, ahadi yoyote itakayofanywa na yeye, akiwa katika utendaji wa kawaida wa uwakala, utendaji huo utakuwa ni halali

mwenye mali
katika
mkataba
unaoweza
kubatilika

kama vile ameruhusiwa na mmiliki wa bidhaa kufanya hivyo;
Isipokuwa kwamba mtoa rehani amefanya kwa nia njema na wakati wa kufanya hivyo hakufahamu kuwa muweka rehani hakuwa na mamlaka ya kufanya hivyo.

(2) Pale ambapo wakala wa biashara anatoa nyaraka za bidhaa kama dhamana, dhamana hiyo itatambulika kama dhamana kwa bidhaa.

(3) Pale ambapo mtoa rehani anamiliki bidhaa aliyoitolea ahadi katika mkataba unaoweza kubatilika chini ya kifungu cha 19, lakini mkataba ulikuwa haujavunjwa wakati ahadi inatolewa, muweka rehani anakuwa na nafasi nzuri ya kumiliki bidhaa iliyowekwa dhamana; ilimradi anafanya kwa nia njema na bila ya kuwa na taarifa ya ya tatizo la umiliki kwa mtoa rehani.

Sura ya 214

(4) Katika kifungu hiki neno "wakala wa biashara" na "nyaraka za bidhaa" vitakuwa na maana kama iliyokusudiwa kwenye Sheria ya Uuzaji wa Bidhaa.

Ahadi ikiwa
muweka
rehani ana
faida ndogo

131. Mtu anapotoa ahadi ya mali ambayo ana maslahi kidogo katika dhamana hiyo, ahadi inakuwa halali kwa kiasi kile cha maslahi hayo.

Mashauri ya mdhamini au mdhaminiwa dhidi ya wafanya waovu

Shauri la
mdhamini au
mdhaminiwa
dhidi ya
mtenda waovu

132. Iwapo mtu wa tatu, kwa makosa, anamyima mdhaminiwa matumizi au umilki wa bidhaa zilizowekwa dhamana, au akimdhuru kwa namna yoyote, mdhaminiwa anastahili kudai nafuu ambazo mwenye bidhaa angedai kama udhamini ungekuwa wa udanganyifu; na mdhamini au mdhaminiwa anaweza kufungua kesi dhidi ya mtu wa tatu.

Mgawanyo wa
nafuu au fidia
inayopatikana
katika
mashauri hayo

133. Chochote kinachopatikana kama unafuu au fidia katika shauri lolote baina ya mdhamini na mdhaminiwa, kitashughulikiwa kulingana na maslahi husika

SEHEMU YA X UWAKALA

Uteuzi na mamlaka ya Wakala

- Tafsiri ya "wakala" na "mhusika mkuu" **134.** "Wakala" ni mtu aliyeajiriwa kufanya kitu chochote kwa niaba ya mwingine, au kumuwakilisha mtu mwingine katika shughuli mbalimbali zinazohusu watu wengine, mtu ambaye anafanyiwa shughuli hizo au anayewakilishwa anaitwa "mhusika mkuu".
- Nani anaweza kuajiri wakala **135.** Mtu yeyote ambaye ana umri wa mtu mzima kulingana na sheria, na ambaye ana akili timamu anaweza kuajiri wakala.
- Nani anaweza kuwa wakala **136.** Kati ya mhusika mkuu na watu wa tatu mtu yeyote anaweza kuwa wakala; lakini mtu mwenye umri mdogo na mwenye matatizo ya akili hawezi kuwa wakala, ambaye atawajibika kwa mhusika mkuu kulingana na vifungu vya sheria hii.
- Malipo siyo muhimu **137.** Hakuna malipo ya awali yanayotakiwa kuanzisha uwakala.
- Mamlaka ya wakala yaweza kuwa ya kutajwa wazi wazi au ya kumaanisha **138.** Mamlaka ya wakala yanaweza kuwa ya kutajwa waziwazi au ya kumaanisha.
- Tafsiri ya mamlaka ya kutajwa waziwazi au ya kumaanisha **139.** Mamlaka inakuwa ya wazi inapotolewa kwa maneno ya kutamka au kwa maandishi na ya kumaanisha pale yanapohusishwa na mazingira; na kitu kinachotamkwa au kuandikwa, au katika hali ya mchakato wa kawaida inahesabiwa ni katika mazingira ya kesi.
- Ukubwa wa mamlaka ya wakala **140.**-(1) Wakala mwenye mamlaka ya kufanya kitu, ana mamlaka ya kufanya vitu vyote halali ambavyo ni muhimu katika kufanya jambo hilo.
(2) Wakala mwenye mamlaka ya kufanya shughuli yoyote ana mamlaka ya kufanya kitu chochote halali, au ambacho mara nyingi kinafanywa katika shughuli hiyo.
- Mamlaka ya wakala wakati wa dharura **141.** Wakati wa dharura, wakala ana mamlaka ya kufanya kitu chochote kwa ajili ya kumlinda mhusika mkuu, kama ambavyo ingefanywa na mtu wa kawaida mwenye busara, katika hali kama ile.

Msaidizi wa Wakala

- Wakati ambapo **142.** Wakala hawezi kuajiri mtu mwingine kutekeleza majukumu ambayo anatakiwa atekeleze isipokuwa katika utamaduni wa kawaida wa

wakala hawezi kukasimu shughuli husika, au aina ya uwakala, wakala msaidizi lazima aajiriwe.

Tafsiri ya "msaidizi wa wakala" **143.** "Wakala msaidizi" ni mtu aliyejiriwa na, na kufanya kazi chini ya usimamizi wa wakala katika shughuli za uwakala.

Uwakilishi wa mhusika mkuu na msaidizi wa wakala aliyeteuliwa **144.**-(1) Pale ambapo wakala msaidizi anateuliwa kihalali, kuhusiana na mtu wa tatu, mhusika mkuu anawakilishwa na wakala msaidizi, anawajibishwa na matendo yake, kama vile ni wakala aliyeteuliwa na mhusika mkuu.

(2) Wakala anawajibika kwa mhusika mkuu kwa matendo ya wakala msaidizi.

(3) Wakala msaidizi anawajibika kuhusiana kwa matendo yake kwa wakala, na siyo mhusika mkuu, isipokuwa kama kuna udanganyifu.

Jukumu la wakala kwa msaidizi wake ambaye hakuteuliwa na mamlaka **145.** Pale ambapo wakala anaajiri msaidizi bila ya kuwa na mamlaka ya kufanya hivyo, wakala anabaki na nafasi yake kwa mhusika mkuu, na anawajibika kwa mhusika mkuu na kwa mtu wa tatu; mhusika mkuu hawakilishwi na wala hawajibiki kwa vitendo vya mtu aliyejiriwa, na wala mtu huyo hawajibiki kwa mhusika mkuu.

Uhusiano kati ya mhusika mkuu na mtu aliyeteuliwa kuwakilisha shughuli za wakala **146.** Pale ambapo wakala anakuwa na mamlaka iliyotajwa waziwazi au ya kumaanisha ya kuajiri mtu mwingine kufanya shughuli kwa niaba ya mhusika mkuu, mtu huyo anakuwa ameteuliwa kwa halali, sio wakala msaidizi, bali na wakala wa mhusika mkuu kwa shughuli hiyo iliyokusudiwa.

Wajibu wa wakala kumtaja aliyeteuliwa **147.** Katika kuchagua wakala wa mhusika mkuu, wakala anatakiwa kutumia juhudi zake zote ambazo mtu wa kawaida angetumia; na kama akifanya hivyo basi hatowajibishwa kwa mhusika mkuu kwa matendo au uzembe utakaokuwa umejitokeza.

Uthibitisho

Haki ya mtu ambaye amefanyiwa kitendo bila ya ruhusayake na matokeo ya uthibitisho **148.** Pale ambapo vitendo vimefanywa na mtu kwa niaba ya mwingine, lakini bila ya kujua au mamlaka yake huyo mtu anaweza kuamua kuthibitisha au kutokutambua vitendo hivyo, na matokeo yatafanana kama ametenda mwenyewe.

Uthibitisho unaweza kuwa wa moja kwa moja au wa kimazingira **149.** Uthibitisho unaweza kuwa wa wazi au wa kumaanisha kwa upande wa mtu ambaye kitendo kimefanywa kwa niaba yake.

Taarifa muhimu kwa uthibitisho **150.** Hakuna uthibitisho halali unaoweza kufanywa na mtu ambaye ufahamu wake wa mambo muhimu hautoshi.

Madhara ya kuthibitisha matendo yasiyostahili yakiwa na sehemu ya mkataba **151.** Mtu anayethibitisha kitendo kisichoruhusiwa kifanywe kwa niaba yake anathibitisha mchakato wote ambao kitendo hicho ni sehemu.

Uthibitisho wa matendo yasiyostahili haumduru mtu wa tatu **152.** Kitendo kinachofanywa na mtu kwa niaba ya mtu mwingine, bila ya ruhusa ya huyo mtu mwingine, kitendo ambacho kama kingefanywa kwa ruhusa, kingemsababishia madhara mtu wa tatu, au kingesitisha haki au maslahi, hakiwezi kuthibitishwa.

Kufutwa kwa Uwakala

Kusitishwa kwa uwakala **153.** Uwakala unasitishwa na mhusika mkuu akiondoa mamlaka yake; au wakala kuacha shughuli za uwakala; au shughuli za uwakala zikikamilika; au kufariki kwa mhusika mkuu au wakala kutokuwa na akili timamu au kutangazwa kuwa ni mufilisi kwa kupitia sheria ya nchi.

Kusitishwa kwa uwakala, ikiwa wakala anamaslahi katika kitu husika **154.** Ikiwa wakala mwenyewe ana maslahi kwenye mali inayosababisha uwakala, uwakala hauwezi kufutwa kwa sababu hii hadi pawepo mkataba.

Wakati ambao mwenye mali anaweza kufuta mamlaka ya wakala **155.** Mhusika mkuu, mbali na kifungu cha 154, anaweza kusitisha uwakala wakati wowote ikiwa mamlaka aliyotoa hayajatekelezwa na kumbana mhusika mkuu.

ufutajio ikiwa **156.** Mhusika mkuu hawezi kufuta mamlaka aliyompa wakala baada

mamlaka yametekelezwa a nusu ya sehemu ya mamlaka hayo kuwa yametekelezwa, ikiwa vitendo na majukumu yalitekelezwa katika nafasi ya uwakala.

Fidia kwa ufutaji uliofanywa na mhusika mkuu au kujitoa kwa wakala **157.** Ikiwa kuna mkataba wa kuandaliwa au wa dhana kwamba wakala ataendelea kwa wakati kwa kipindi chochote, mhusika mkuu ni lazima amlipe fidia wakala, au wakala amlipe mhusika mkuu inategemea na jambo lilivyo, kwa kufuta au kujitoa uwakala bila ya sababu za msingi.

Taarifa ya ufutaji au rudisho **158.** Muda wa kutosha kwa taarifa ya ufutaji au rudisho lazima utolewe; vinginevyo madhara yatakayojitokeza kwa kuto fanya hivyo yatafidiwa na mwingine.

Ufutaji na rudisho vyawezakuwa vya kutajwa wazi au kwa kumaanisha **159.** Ufutaji na rudisho vinaweza kuwa kwa kutajwa wazi au kwa kumaanisha matendo ya mhusika mkuu au wakala.

Wakati kusitishwa kwa mamlaka ya wakala kutaleta madhara kwa wakala na kwa mtu wa tatu **160.** Kusitisha kwa mamlaka ya wakala hakutakuwa na nguvu hadi taarifa itakapomfikia wakala au mtu watatu.

Jukumu la wakala wakati wa kusitisha uwakala kutokana na kifo cha mhusika mkuu au kupungukiwa akili **161.** Pale ambapo uwakala unasitishwa kwa kufariki kwa mhusika mkuu au kuwa na matatizo ya akili, kwaniaba ya wawakilishi wa mhusika mkuu, wakala anatakiwa kuhakikisha anatumza maslahi yake katika jambo husika.

Kusitishwa kwa mamlaka ya uwakala msaidizi **162.** Kusitisha kwa mamlaka ya wakala kunasababisha pia kusitishwa kwa wakala msaidizi aliyeajiriwa naye, kufuatana na kanuni zilizopo kuhusiana na usitishaji wa mamlaka ya uwakala.

Wajibu wa wakala kwa mhusika mkuu

- Wajibu wa wakala katika kutekeleza shughuli za mhusika mkuu **163.** Wakala ana jukumu la kutekeleza shughuli za mhusika mkuu kulingana na maelekezo yanayotolewa na mhusika mkuu, au kama hakutakuwepo na maelekezo hayo yoyote kulingana na taratibu za kutekeleza shughuli hiyo. wakala anapofanya vinginevyo anatakiwa awajibike kwa mhusika mkuu kwa hasara yoyote itakayopatikana, na kama akipata faida basi aseme imepatikana vipi.
- Ujuzi na uadilifu unaotakiwa kwa wakala **164.** Wakala analazimika kutekeleza majukumu ya uwakala kwa umakini mkubwa kama ambavyo anafanya mtu mwingine wa kawaida isipokuwa tu kama mhusika mkuu ameweka vigezo. Wakati wote wakala anatakiwa kutenda kwa umakini na kutumia utaalamu wake katika shughuli husika; na kumlipa fidia mhusika mkuu kwa hasara atakayoisababisha kwa uzembe au kukosa utaalamu lakini sio kwa hasara iliyojificha iliyosababishwa na uzembe au tabia mbaya.
- Akaunti ya wakala **165.** Wakala anatakiwa kutoa mahesabu kwa mhusika mkuu pindi anapoagizwa kufanyahivyo.
- Jukumu la wakala kuwasiliana na mhusika mkuu **166.** Wakati wa dharura ni wajibu wa wakala kufanya juhudi kuwasiliana na mhusika mkuu na kupata maelekezo kutoka kwake.
- Haki ya mhusika mkuu wakati wakala akifanya kazi bila ridhaa ya mhusika **167.** Iwapo wakala anafanya shughuli kwa mamlaka yake mwenyewe bila ya kupata ridhaa ya mhusika mkuu na kupata ufahamu wake, mhusika mkuu anaweza kukataa mchakato mzima wa shughuli alizozifanya wakala kama itagundulika kwamba kuna jambo limefichwa na wakala au kwamba shughuli za wakala hazina faida kwake yeye mhusika mkuu.
- Haki ya mhusika katika manufaa aliyoyapata wakala katika shughuli zake za uwakala **168.** Iwapo wakala anashughulika kwa nafasi ya uwakala bila ya ufahamu wa mhusika mkuu, basi mhusika mkuu ana haki ya kudai faida yoyote inayoweza kusababishwa na shughuli hiyo.
- Haki ya wakala ya kubakiza pesa **169.** Katika malipo ya kazi anayoyapata, wakala anaweza kubakiza pesa za gharama alizoziingia wakati wa kutekeleza shughuli hiyo, na pia kipato chake kama wakala.

kwenye
akaunti ya
mhusika.

Wajibu wa
wakala kulipa
pesa
iliyopatikana
kwa mhusika

170. Wakala anatakiwa kumlipa mhusika mkuu pesa zote alizozipata ,akizingatia makato yanayohusika yaliyofanyika

Wakati malipo
ya wakala
yanakuwa
tayari

171. Kama hakutakuwepo mkataba wowote maalum, malipo ya shughuli yoyote hayataweza kufanyika mpaka shughuli hiyo ikamilike; lakini wakala anaweza kubakiza pesa aliyolipwa kwa mauzo ya bidhaa aliyoyafanya hata kama sio bidhaa zote ziumeuzwa, au hata kama mauzo hayajakamilika.

Wakala
hastahili
malipo kwa
kazi
aliyoharibu

172. Wakala ambaye atakuwa na utovu wa nidhamu katika shughuli za uwakala hastahili kupata ujira wowote kwa sehemu ile ya shughuli aliyoikosea.

Rehani ya
wakala kwa
mali ya
mhusika mkuu

173. Bila ya kuwepo kwa mkataba wowote maalum, wakala anastahili kubakia na bidhaa, nyaraka au bidhaa yoyote, inayohamishika au isiyohamishika, ya mhusika mkuu ambayo anayo yeye mpaka pesa yake ya posho ya kamisheni, malipo na huduma kwa shughuli alizozifanya itakapokuwa imetolewa.

Wajibu wa mhusika mkuu kwa Wakala

Wakala
anatakiwakuli
pwa kwa kazi
halali
anazozifanya

174. Mwachiri wa wakala analazimishwa kumlipa wakala kwa mambo yote mazuri aliyoyafanya kwa nafasi yake kama wakala.

Wakala
anatakiwa
alipwe kwa
kazi halali
anazozifanya
kwa nia njema

175. Mtu anapoajiri mwingine kwa ajili ya kumfanyia shughuli, na wakala anafanya shughuli hiyo kwa nia njema, mwajiri ana wajibu wa kumlipa fidia wakala dhidi ya madhara au matokeo ya kitendo hicho, ingawa ilisababisha madhara kwa haki za mtu wa tatu.

Si kosa la
mwajiri wa
wakala

176. Pale ambapo mtu anamwajiri mwingine kufanya shughuli ambayo ni jinai, mwajiri hawajibiki kwa wakala, iwe kwa maneno au kwa mazingira ya ahadi, kuwa atamfidia dhidi ya matokeo ya kitendo hicho.

kufanya jinai

Fidia kwa
madhara
aliyoyapata
wakala
kutokana na
uzembe wa
mhusika

177. Mhusika mkuu lazima alipe fidia kwa wakala wake kwa madhara yaliyosababishwa na wakala kutokana na wakala kukosa utaalim.

Matokeo ya Uwakala katika Mkataba na Mtu wa Tatu

Kutekeleza na
matokeo ya
mikataba ya
uwakala

178. Mikataba inayosainiwa na wakala, na majukumu yanayo tokana na vitendo vya wakala, yanaweza kutekelezwa kisheria kwa namna ile ile, na vinaweza kuwa na matokeo ya kisheria kama vile mkataba na matendo yamefanywa na vimefanywa na mhusika mkuu.

Nafasi ya
mhusika mkuu
pale wakala
anapovuka
mipaka ya
mamlaka

179. Wakati ambapo wakala anatekeleza zaidi ya aliyoruhusiwa kufanya, na kama aliyoyafanya kwa mamlaka yake yanaweza kutengeka kutoka na kwa yale ambayo hakuwa na mamlaka nayo, yale aliyoyafanya ndani ya himaya yake yanawafunga yeye wakala na mhusika mkuu.

Mhusika mkuu
hawajibiki
ikiwa uvukaji
mipaka wa
wakala
ulikuwa
hautabiriki

180. Wakati ambapo wakala anatekeleza zaidi ya aliyotakiwa kufanya, na yale aliyoyazidisha hayawezi kutenganishwa na yaliyokuwa ndani ya mipaka yake ya kazi, mhusika mkuu halazimishwi kutambua shughuli hiyo.

Matokeo ya
taarifa
apewayo
wakala

181. Taarifa yoyote inayotolewa kwa wakala au maelezo yanayopatikana kwake, ikiwa inapatikana katika mchakato wa kazi baina yake na mhusika mkuu, yanakuwa na nguvu ya kisheria kwa mtu wa tatu kama ambavyo inakuwa kwa mhusika mkuu.

Wakala kwa
nafsi yake
hawezi
kulazimishwa
wala kubanwa
na mikataba
kwa niaba ya
mhusika mkuu

182. (1) Kama hakutakuwepo na mkataba wowote, wakala hawezi kulazimisha yeye binafsi kutekelezwa kwa mkataba alioingia yeye kwa niaba ya mhusika mkuu, na wala hafungwi nao pia.

(2) Mkataba uliotajwa katika kifungu kidogo cha (1) utadhaniwa kuwepo katika mazingira yafuatayo:-

(a) pale ambapo mkataba umetengenezwa na wakala kwa mauzo au

- ununuzi wa mali ya mfanya biashara aishiye nje ya nchi;
- (b) pale ambapo wakala hajataja jina la mhusika mkuu wake;
 - (c) pale ambapo mhusika mkuu ametajwa na hawezi kushitakiwa.

Haki za
wahusika
katika
mkataba
uliofanywa na
wakala
hazitakiwi
kuwekwa
bayana

183.-(1) Iwapo wakala anafanya mkataba na mtu ambaye ama hakujua au ana sababu ya kumhisi kuwa ni wakala, mhusika mkuu anaweza kudai utekelezaji wa mkataba; lakini upande mwingine wa mkataba unakuwa na haki dhidi ya wakala kama vile wakala angekuwa mhusika mkuu.

(2) Iwapo mhusika mkuu amejitambulisha kabla ya mkataba kukamilika, upande mwingine wa mkataba unweza kukataa kutekeleza mkataba, kama anaweza kuonyesha kwamba, kama angemfahamu mhusika mkuu kwenye mkataba, au kama angemfahamu kuwa wakala sio mhusika mkuu, asingeingia kwenye mkataba.

Haki ya mtu
anayefanya
kazi na wakala
aliyekosea

184. Katika kesi ambapo wakala mwenyewe anakuwa na hatia, mtu anayeshughulika nae anaweza kumuwajibisha wakala au mhusika mkuu au wote.

Matokeo ya
kumtumia
wakala au
mhusika mkuu

185. Wakati mtu aliyefanya mkataba na wakala na kumshawishi kuwa ni mhusika mkuu pekee ndio atawajibika, au akamshawishi mhusika mkuu kufanya kazi kwa madai kwamba wakala ndiye atakayewajibishwa, hawezi kuwajibisha wakala wala mhusika mkuu.

Kosa la
kuigiza
uwakala

186. Mtu akiongopa kuwa yeye ni wakala aliyekubalika, na kumshawishi mtu wa tatu kufanya nae biashara kama wakala, mtu huyo anakuwa amekosea, kama mwajiri wake hatorekebisha vitendo vyo wakala, kwa kumlipa fidia mlengwa kwa madhara aliyoyapata kutokana na kufanya nae kazi.

Mtu mwenye
mkataba wa
uongo wa
uwakala
hatakiwi
kuhusishwa na
utekelezaji

187. Mtu ambaye mkataba umefanyika dhidi yake kwa nafasi ya wakala haruhusiwi kudai utekelezaji wake kama alikuwa akitekeleza kwa nafasi yake na siyo wakala.

Kosa kwa
mhusika mkuu
kulazimisha

188. Wakati ambapo bila ya kuwa na mamlaka, wakala anafanya jambo au anajipa majukumu kwa mtu wa tatu kwa niaba ya mhusika mkuu, mhusika mkuu anabanwa na kitendo hicho ikiwa kwa matendo au maneno

imani kwamba amemshawishi mtu wa tatu kuamini kwamba vitendo vile vile ndani ya wakala mamlaka ya wakala.
aliruhusiwa
kufanya
vitendo
alivyofanya
bila ruhusa

Matokeo ya udanganyifuu
wakilishi wa uongo katika makubaliano a

189. Uwakilishi wa uongo na udanganyifu unaofanywa na wakala akiwa anatekeleza wajibu wake kwa nafasi ya mhusika mkuu, una madhara sawa katika makubaliano yaliyofanywa na wakala kama vile udanganyifu umefanywa na mhusika mkuu, lakini udanganyifu uliofanywa na wakala kwa jambo ambalo halipo katika mamlaka yake haumdhuru mhusika mkuu.

SEHEMU YA XI UBIA

Asili ya Ubia

Tafsiri ya "ubia" na "ushirika"

190.-(1) "Ubia" ni uhusiano uliopo baina ya watu wanaofanya biashara kwa pamoja ambayo inazalisha faida.

(2) Mtu aliyeingia ubia na mwingine wanaitwa kwa umoja wao "shirika", na jina wanalolitumia kwenye biashara ni "jina la shirika".

Kanuni za kujulisha kuwepo kwa ubia

191.-(1) Mahusiano ya ubia yanatokana na mkataba na siyo wadhifa.
(2) Katika kuamua kama kundi la watu ni wabia au siyo, uzito utawekwa katika kanuni zifuatazo-

- (a) upangaji wa pamoja, upangaji unaofanana, mali za pamoja, mali zinazofanana au umiliki wa sehemu tu hausababishi ubia kwa mali yoyote waliyonayo, iwe mpangaji au mmiliki wanagawana au la faida wanayoipata mahali pale;
- (b) kugawana mapato ya mwisho pekee hakisababishi ubia, iwe wanaogawana mapato hayo wana haki za pamoja au la, au maslahi ya pamoja katika mali ambayo malipo ya mwisho yanatolewa;
- (c) kupatikana kwa faida ya mtu mwenye hisa katika biashara ni ushahidi wa awali kuwa ni mbia katika biashara, lakini upatikanaji huo wa hisa au malipo yoyote kulingana na faida ya biashara, yenyewe peke yake hayamfanyi awe mbia katika biashara, na zaidi upatikanaji huo wa hisa au malipo-
 - (i) kwa kutoa mkopo kwa mtu aliyeingia au anayetegemea kuingia kwenye biashara;
 - (ii) kwa mtumishi au wakala kama ujira;

- (iii) kwa mjane au mtoto wa marehemu mwenye ubia kama kiinua mgongo; au
- (iv) kwa mmiliki wa zamani au mmiliki wa sehemu ya biashara, kama malipo ya mauzo ya hisa, havimfanyi mpokeaji awe mbia na mtu anayefanya biashara.

Mahusiano baina ya Wabia

Majukumu ya jumla kwa wabia

192. Wabia wanatakiwa wafanye biashara ya ubia kwa kusudio la faida kubwa, wawe na busara na waaminifu miongoni mwao, na kutoa mahesabu ya kweli na taarifa za vitu vyote vinavyohusu ubia kwa mbia au wawakilsih wake wa kisheria.

Ridhio la kutofautiana katika masharti ya ubia

193. Haki za hiyari na wajibu wa wabia, iwe zimetajwa kwenye makubaliano au sheria hii, zinaweza kubadilishwa kwa ridhaa ya wabia wenyewe, na ridhaa hiyo inaweza kuwa ya wazi au yakudhaniwa kulingana na shughuli husika.

Ufanyaji wa shughuli na haki za msingi na majukumu

194. Bila ya kuwepo kwa mkataba wowote, haki na wajibu wa wadau kuhusiana na ubia zitatambuliwa kwa kanuni zifuatazo-

- (a) kila mbia ana haki ya kuwa ni sehemu ya uongozi katika shughuli za ubia;
- (b) tofauti yoyote itakayojitokeza katika hali ya kawaida inayohusu shughuli za ubia inaweza kuamuliwa na wabia walio wengi, lakini hakutafanywa mabadiliko yoyote kuhusiana na ubia katika biashara bila ya ridhaa ya wabia wote waliopo;
- (c) kila mbia ana haki ya kuon, kukagua na kunakili kitabu chochote cha shirika;
- (d) Mbia hatastahili ujira kwa kushiriki katika kutimiza shughuli za shirika;
- (e) Wabia wote wanastahili kugawana sawa mtaji na faida ya biashara, na kuchangia sawa penye upotevu wa shirika;
- (f) Shirika litamrejeshea kila mbia malipo na gharama zingine alizoingia-
 - (i) katika mazingira ya kawaida ya biashara za shirika; na
 - (ii) kitu chochote cha msingi kilichofanywa kunusuru biashara au mali za shirika;
- (g) Mbia atafidia shirika hasara yoyote atakayoisababisha kwa udanganyifu au uzembe wa makusudi katika kutekeleza shughuli za shirika.

Mali za ubia

195.-(1) Mali zote na haki na maslahi dhidi ya mali zilizoletwa kwenye stoo ya ubia au ailizopatikana kwa kununua au vinginevyo, kwa niaba ya

shirikai, kwa sababu au kwa manufaa ya ubia, ikiwemo nia njema ya biashara, ni mali za ubia na lazima zitunzwe na wabia kwaajili ya ubia wao kulingana na makubaliano ya ubia au vifungu vya sheria hii.

(2) Labda iwe kuna nia nyingine, mali na haki na maslahi dhidi ya mali iliyopatikana kwa pesa ya shirika vitahesabiwa kuwa vimenunuliwa kwa akaunti ya shirika.

(3) Ikiwa aridhi au mali yoyote inayoweza kurithiwa imekuwa ni mali ya ubia, kama kutakuwa na nia ingine, vitashughulikwa miongoni mwa wabia (ikiwa ni pamoja na wawakilishi wa wabia waliofariki), na pia kati ya warithi na wasimamizi.

Jukumu la wabia katika faida binafsi na ya biashara

196. Kufuatana na uwepo wa mkataba baina wa wabia-

- (a) iwapo mbia anapata faida yoyote kutokana na shughuli za shirika, au kutokana na kutumia mali au biashara inayolihusu shirika au jina la shirika, anatakiwa ajulishe faida aliyopata na kulipa shirika;
- (b) Ikiwa mbia anafanya biashara inayofanana au kushindana na shirika, bila ya kuwa na ridhaa ya wabia wengine, atataja faida na kulilipa shirika kwa faida yote aliyopata katika biashara.

Neno ubia linapokosa nguvu

197. Kama ubia utaingia katika masharti ya kudumu na kuendelea baada ya muda kuisha, haki na wajibu wa wabia vitabakia kama awali kama hakutakuwa na makubaliano yoyote, haki na wajibu huo utatumika kwa wabia watakaojivua kwa hiyari.

Utambulisho wa wabia wapya

198. Ikiwa kutakuwepo na mkataba kati ya wabia, mtu hatotambulishwa kuwa mbia katika shirika bila ya kuwepo kwa ridhaa ya wabia wengine wote.

Kukataliwa

199. Mbia hawezi kufukuzwa na wabia wengine katika shirika isipokuwa tu kama wabia walishakubaliana kufanya hivyo kwa maandishi.

Kustaafu

200. Kama hakuna masharti yamekubaliwa kwa muda wa mtu kuwa mbia, mbia yeyote anaweza kuamua ubia wake kwa kutoa taarifa kwa wabia wengine.

Mahusiano ya Wabia kwa wanaofanya nao kazi

Nguvu ya wabia kufunga shirika

201.-(1) Kila mbia ni wakala wa shirika na wabia wengine kuhusiana na shughuli za ubia; na kitendo cha kila mbia ambaye anayefanya shughuli za kawaida za biashara za shirika zinalifunga shirika na wabia wengine, isipokuwa tu mbia anayefanya kitendo hana mamlaka kufanya hivyo, na mtu mwenye shughuli anajua kuwa hana mamlaka au hakuajua au hakuamini kuwa yeye ni mbia.

(2) Bila ya kuwepo kwa mila na mazoea ya biashara au mamlaka ya kuifanyia kazi shirika, mbia sio wakala wa shirika au wengine kwa-

- (a) kupeleka matatizo yanayohusu shirika kwenye usuluhishi;
- (b) kufungua akaunti ya benki kwa niaba ya shirikai;
- (c) kubembeleza ama kusuluisha malalamiko au sehemu ya malalamiko ya shirikai;
- (d) kufuta kesi au masuala yoyote yaliyofunguliwa mahakamani kwa niaba ya shirika;
- (e) kukubali matatizo kwenye shauri dhidi ya shirika;
- (f) kujipatia mali isiyohamishika kwa niaba ya shirikai;
- (g) kuhamisha mali zinazomilikiwa na shirika;
- (h) kuingia kwenye ubia kwa niaba yashirika.

Wabia
kufungwa na
vitendo vyao
kwa niaba ya
shirikai

202. Kitendo au kitu kinachohusiana na shirika kinachofanywa au kutekelezwa kwa jina la shirika, au kwa namna nyingine yoyote ikionyesha nia ya kulibana shirika, kwa mtu yeyote mwenye mamlaka ya kufanya hivyo, awe mbia au la, anabanwa na shirika na wabia wengine:

Isipokuwa kwamba hakuna kitu chochote kitakachodhuru kanuni za utawala wa sheria kuhusiana na utekelezaji wa mambo au nyaraka za kifedha.

Jukumu la
wabia
kuhusiana na
madeni

203. Kila mbia anawajibika kwa madeni na wajibu alioupata akiwa kama mbia katika shughuli za kawaida za ubia au kwa niaba ya ubia.

Deni kwa
makosa na
matumizi
yasiyo halali

204. Kila mbia anatakiwa kulipa fidia kwa mtu wa tatu kuhusiana na hasara au uharibifu wa adhabu aliyoipata-

- (a) kwa kitendo kibaya au mbia kuacha kufanya kile alichotakiwa kufanya kwa shughuli za shirika, au kwa mamlaka ya wabia wengine;
- (b) kwa matumizi yoyote mabaya ya pesa yoyote au mali ambapo mbia amefanya nje ya upeo wa mamlaka;
- (c) kwa matumizi yoyote mabaya yaliyofanywa na mbia mmoja au wengi, ya pesa au mali ya shirika vikiwa chini ya himaya ya shirika.

Matumizi
mabaya ya
mali kwa ajili
ya ubia

205. Kama mbia, chini ya udhamini, kinyume na matarajio akatumia mali au pesa za wabia, hakuna mbia atakayekuwa na hatia dhidi ya walionufaika:

Isipokuwa kwamba-

- (a) kifungu hiki hakitahusisha na matatizo atakayoyapata mbia yeyote kwa sababu ya kuwa ta taarifa ya kuvunjika kwa udhamini;
- (b) kifungu hiki hakitazuia pesa za udhamini kufuatiliwa na kupatikana kutoka kwenye shirika kama bado iko chini ya himaya yake.

Kosa kujifanya kuwa na madaraka

206. Kila mmoja ambaye kwa maneno au kwa maandishi au kwa vitendo amejitangaza kuwa ni mbia, au ambaye anajua ameathirika kwa kuwakilishwa kama mbia katika shirika fulani, anawajibika kama mbia kwa mtu yeyote mwenye imani na uwakilishi huo unaoleta tija kwenye shirika, iwe uwakilishi huo amejulishwa mtu anayetoa mali au la, au akiwa na ufahamu wa kutengeneza ubia:

Isipokuwa kwamba, baada ya kifo cha mbia, shughuli za ubia zinaendelea kwa jina la zamani la kampuni, kuendelea kutumia jina hilo au la marehemu haisababishimali za wasimamizi kuwa sehemu ya deni lolote la ubia wowote ulilojitokeza baada ya kifo.

Taarifa kwa wadau kuwa taarifu kwa shirika

207. Taarifa kwa mbia yeyote ambaye kwa kawaida anajihusisha na shughuli za ubia kuhusu suala lolote la mambo ya ubia itafanyakazi kama taarifa kwa shirika, isipokuwa katika mazingira ya udanganyifu wa shirika kwa ridhaa au bila ya ridhaa ya mbia.

Madeni kwa wabia wanaoondoka na wanaoingia

208.-(1) Mtu aliyepokelewa kuwa mbia katika shirika lililokwisha kuwepo hawezi kuwajibika kwa wadau wa shirika kwa kitu chochote walichokifanya kabla ya kuwa mbia.

(2) Mbia aliyeacha kuwa mbia katika shirika hawezi kuacha kuwajika kwa madeni ya shirika yaliyojitokeza kabla ya kustaafu kwake au kujitoa.

(3) Mbia anayestaafu, kwa makubaliano baina yake na wajumbe wa shirika, anaweza kusamehewa madeni yake. Makubaliano yanaweza kuwa ya moja kwa moja au yakudhaniwa kulingana na utendaji wa mdaiwa na shirika husika.

Ufutaji wa wadhamini endelevu kwa kubadili jina la shirika

209. Udhamini unaoendelea, unaotolewa kwa shirika au mtu wa tatu, kuhusiana na shughuli za shirika, bila ya kuwepo kwa mkataba mwingine, unaweza ukasitishwa kwa shughuli za baadae kwa kubadilisha katiba ya shirika ambayo, au kuhusu mchakato ambao udhamini huo unahusika.

Haki ya waliogawa sehemu katika ubia

210.-(1) Kutolewa kwa sehemu ya mbia katika ubia, iwe moja kwa moja au kwa kuweka rehani au mali itakayorejeshwa, dhidi ya wabia wengine, wakati ubia ukiendelea, hakumpi nafasi aliyepokea mali kuingilia utawala au utendaji wa shughuli za ubia au kutaka mahesabu yoyote yaliyofanywa katika shughuli za ubia, au kukagua vitabu vya mahesabu, lakini kunamfanya mpokeaji wa mali hiyo aweze kupata sehemu ya faida ambayo mtoaji angestahili, na mpokeaji lazima akubali mahesabu ya faida yaliyokubaliwa na wabia wengine.

(2) Katika kesi ya kuvunjika kwa ubia, iwe kwa ridhaa ya wabia wote au wabia walio kasmiwa, mpokeaji anastahili kupata sehemu ya mali za ubia ambazo mtoaji anastahili baina yake na wabia wengine, na kwa ajili ya kuthibitisha sehemu hiyo kwa ajili ya mahesabu kuanzia tarehe ya kuvunjika.

Watoto
hawaruhusiwi
kuwa wabia

211. Mtu ambaye ni mdogo kulingana na sheria inayotumika mahali alipo hastahili kuwa mbia katika shirika.

Kuvunjika kwa ubia na Matokeo yake

Kuvunjika
kutokana na
kwisha kwa
muda au kwa
kutoa taarifa

212.-(1) Mbali na kuwepo kwa mkataba wowote baina ya wabia, ubia unaweza kuvunjika-

- (a) iwapo ulifanyika kwa kipindi maalum na kwa kufikia mwisho wa kipindi hicho;
- (b) iwapoulifanyika kwa mradi mmoja na kwa kufikia mwisho wa mradi huo;
- (c) iwapo ulifanyika kwa kipindi kisicho maalum, na kwa mbia kutoa taarifa ya kusudio la kuvunja ubia.

(2) Pale ambapo ubia umevunjika kwa taarifa kama ilivyo chini ya aya ya (c) ya kifungu kidogo cha (1), ubia unakwisha kuanzia tarehe itakayotajwa kwenye taarifa ya kusitisha ubia, au kama hakuna tarehe iliyotajwa, basi tangu tarehe ya kutoa taarifa.

Kuvunjika
kutokana na
kifo au
kufilisika

213.-(1) Mbali ya kuwepo kwa makubaliano baina ya wabia, ubia unaweza kwisha kwa wabia wote kwa kifo au kufilisika.

(2) Kwa ridhaa ya wabia wengine, ubia unaweza kuisha ikiwa sehemu ya mbia yeyote katika mali ya ubia itakuwa mashakani chini ya kanuni ya 48 ya amri ya 21 ya Jedwali la kwanza la Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai.

Sura ya 33

Kuvunjika
kwa ubia
kinyume na
sheria

214. Katika hali yoyote ubia unaweza kuvunjika kwa kutokea kwa jambo lolote kinyume na sheria na kusababisha shughuli za shirika kushindwa kufanyika au wajumbe kushindwa kuendeleza ubia wao.

Kuvunjika
kwa amri ya
mahakama

215. Kwa maombi ya mbia, mahakama inaweza kutekeleza kuvunjika kwa ubia katika lolote kati ya yafuatayo-

- (a) mbia anapokuwa na matatizo ya akili;
- (b) mbia anaposhindwa kutekeleza wajibu wake katika mkataba wa ubia;
- (c) pale ambapo mbia, mbali na mbia aliyepeleka shauri mahakamani, kulingana na maoni ya mahakama amekuwa na hatia ya kusababisha matendo ya kuhujumu shughuli za ubia;
- (d) pale ambapo mbia, mbali na mbia aliyepeleka shauri mahakamani kwa makusudi na kwa kurudia amekuwa akivunja mkataba wa ubia, au amekuwa akifanya vitendo ambavyo havifanywi na wabia

wengine au kuwakwamisha wengine kufanya shughuli za kuendeleza ubia;

- (e) pale ambapo shughuli za ubia zinafanywa kwa hasara;
- (f) pale ambapo katika kesi yoyote mazingira yamejitokeza kwamba, kulingana na maoni ya mahakama, ni vyema na ni haki ubia uvunjwe.

Haki ya watudhidi ya wajumbe dhahiri wa shirika

216.-(1) Pale ambapo mtu anajishughulisha na shirika baada ya kubadilishwa kwa katiba yake, anatakiwa kuwahudumia wajumbe wote wa shirika kama vile bado ni wajumbe hadi taarifa ya mabadiliko itolewe.

(2) Tangazo katika Gazeti la Serikali itakuwa ni taarifa tu kwa watu ambao hawakuwa na shughuli zozote na shirika kabla ya kuvunjika kwa shirika au kutokea kwa mabadiliko yaliyotangazwa.

(3) Mali za mtu aliyefariki, au aliyefilisika, au mbia ambaye hajulikani na mtu anayejishughulisha na shirika kuwa ni mbia, amestaafu kutoka kwenye shirika, hahusiki na madeni ya shirika yaliyopatikana baada ya kifo chake, ufilisi au kustaafu.

Haki ya wabia ya kupata taarifa ya kuvunjika ubia

217. Katika kuvunja ubia, au kustaafu kwa mbia, mbia yeyote anaweza kutoa taarifa hiyo, na anaweza kumuomba mbia mwingine au wengine kukubaliana na hilo kwa kutenda mambo ambayo ni muhimu na hayawezi kufanyika bila ya wao kukubali.

Muendelezo wa haki na madeni kwa wabia baada ya kuvunjika kwa ubia

218. Baada ya kuvunjika kwa ubia, haki na wajibu wa wabia vitaendelea kwa vitu vyote muhimu katika kukamilisha shughuli za ubia, na kukamilisha michakato iliyoanza lakini haikwisha hadi wakati wa kuvunjika kwa ubia na sio vinginevyo:

Isipokuwa kwamba shirika halibanwi kwa namna yoyote ile na vitendo vya mbia ambaye amekuwa mufilisi; lakini kifungu hiki hakidhuru jukumu la mtu yeyote ambaye, baada ya kufilisiwa, amejiwakilisha kama mbia wa ufulisi au akiwa anajua amejiwakilisha kama mbia mufilisi.

Haki ya mbia katika maombi ya mali za wabia

219. Katika kuvunjika kwa ubia, mbali na wabia wengine katika shirika, na watu wengine wote wanaodai maslahi kama wabia, kila mbia anastahili, kupata mali ya ubia iliyotumika kulipa madeni ya shirika, na kupata ziada ya mali baada ya malipo hayo ili itumike kulipa deni lolote la mbia baada ya kukata deni lolote kwao linalodaiwa na shirika; kwa hiyo kila mbia au mwakilishi wake, wakati wa kusitisha ubia, anaweza kuiomba mahakama ifunge shughuli za shirika.

Uteuzi wa msimamizi ikiwa ubia umevunjika mapema

220. Ikiwa mbia mmoja amelipa malipo makubwa kwa mbia mwingine kwaajili ya kuingia katika ubia wa masharti ya kudumu, na ubia ukavunjika kabla ya muda kuisha kwa vyovyote vile mbali na kifo cha mbia, mahakama inaweza kutoa mari ya kurudishwa kwa malipo yale, au sehemu ya malipo kulingana na itakavyoona, ikitilia maanani masharti ya mkataba wa ubia na muda wa ambao ubia ulidumu isipokuwa -

- (a) kama kuvunjika huko, kulingana na hukumu ya mahakama, kulitokana na matendo ya mbia aliyelipa malipo makubwa, au
- (b) kama ubia umefutwa kwa makubaliano yaliyojumuishia kifungu cha kutaka kurudisha malipo au sehemu ya malipo.

Haki ikiwa ubia umevunjika kwa udanganyifu au uwakilishi mbaya

221. Mkataba wa ubia unapofutwa kwa sababu za udanganyifu au uwakilishi wa uongo kwa upande mmoja wao, bila ya kujali haki ingine yoyote, upande unaostahili kufuta unatakiwa-

- (a) kupata malipo kutoka katika mali za ubia, baada ya kuiridhisha kampuni kwa malipo yoyote aliyoyafanya kwa kununua shea na kuchangia mtaji;
- (b) kuwa katika nafasi ya wadai wa shirika kwa malipo yoyote aliyoyafanya kuhusiana na ubia; na
- (c) kufidiwa na mtu aliyedanganya au aliyewakilisha dhidi ya madeni ya shirika.

Haki ya mbia anayeondoka katika mazingira fulani kuhusiana na faida iliyopatikana baada ya kuvunjika kwa ubia

222. Ikiwa mjumbe yeyote wa shirika amefariki au vyovyote vile ameacha kuwa mbia, na waliobaki wanaendeleza shughuli za shirika na mtaji wake au mali bila ya kufanya mahesabu ya mwisho baina ya shirika na wabia walioondoka au warithi wao, bila ya kuwepo kwa makubaliano mengine, mbia anayeondoka au mrithi wake anastahili sehemu ya faida iliyopatikana, tangu kuvunjika kwa ubia, kama mahakama itakavyoona inafaa kulingana na mchango wake, kwa maslahi ya asilimia tano kwa mwaka katika jumla yake ya sehemu ya ubia:

Isipokuwa kwamba ikiwa katika mkataba wa ubia kuna kuwa na hiyari wa wabia wanaobaki au kuendelea kununua maskahi ya aliyefariki, au mbia anayeondoka, na hiyari hiyo inatekelezwa, mali za mbia aliyefariki, au mbia anayeondoka, au mali zake, kulingana na kesi itakavyokuwa, hastahili malipo zaidi ya faida; lakini ikiwa mbia yeyote anafanya kulingana na hiyari yake na katika hali yoyote hajatimiza masharti, atatakiwa kulipa kulingana na vifungu vingine vinavyofuata.

Sehemu ya
mbia
aliyefariki au
kustaafu
itakuwa deni

223. Mbali na kuwepo kwa mkataba wowote miongoni mwa wadau, kiwango kinachopatikana kutoka kwa wabia waliopo au wabia wanaoendelea kutoka kwa wanaoondoka au wawakilishi wa wabia wanaliyofariki kuhusiana na sehemu za wabia walioondoka au waliyofariki ni deni linaloanzia siku walipojitoa au walipofariki.

Kanuni
kuhusiana na
mgawanyo wa
mali baada ya
kufunga
akaunti

224. Katika kuweka sawa mahesabu wakati wa kuvunja ubia, kanuni zifuatazo, mbali kuwepo kwa mkataba, zitafuliwa-

- (a) kupotea, ikiwemo kupotea na kufilisika kwa mtaji, deni litalipwa kwanza kutokana na faida, inayokaribia mtaji, na mwisho, kama italazimu, litalipwa na wabia wenyewe katika mgawanyo ambao walistahili kuufuata kugawana faida;
- (b) mali za shirika zikiwemo pesa, kama zipo, zilizochangwa na wabia kufidia hasara au kufilisika kwa mtaji, zitatumiwa kwa utaratibu na njia zifuatazo-
 - (i) katika kulipa madeni ya shirika kwa watu ambao sio wabia;
 - (ii) katika kumlipa kila mbia kiwango anacholidai shirika kama nyongeza mbali na mtaji;
 - (iii) katika kumlipa kila mbia kiwango anacholidai shirika kama mtaji;
 - (iv) kinachobakia, kama kipo, kitagawanywa miongoni mwa wabia katika mlinganyo ambao faida inagawanywa.

Ulipaji wa
madeni ya
shirika na
madeni
mengine

225. Inapotokea shirika linadaiwa, na pia wabia wanadaiwa madeni binafsi, mali za shirika zitatumiwa kulipa deni la shirika na kama kutakuwa na ziada, basi, sehemu ya kila mbia itatumika kulipa deni lile; mali binafsi ya kila mbia itatumika kwanza kulipia deni la mbia, na ziada (kama itapatikana) italipa deni la shirika.

Ubia wa
pamoja na
mashirika
yaliyoungana

226. Ubia usio wa kawaida, kama vile ubia wa kuungana na mashirika yenye mali za pamoja, utashughulikiwa na sheria inayotumiwa kwa wakati huo.

SEHEMU YA XII UFUTAJI NA MASHARTI YA VIFUNGU VYA MPITO

Kuto tumika
kwa sheria ya
mikataba ya
India na
marekebisho
yake Sura ya 2

227. [Kutotumika kwa Sheria ya Mikataba ya India na marekebisho ya R.L. Sura ya 2.]

Masharti ya

228. [Masharti ya vifungu vya mpito.]

vifungu vya
mpito